**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**
**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa. |
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi |
| 18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |

| | |
|---|---|
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae |
| 30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 32. Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa |
| 33.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 34.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 35. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 37. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 38.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 44.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 45.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 46.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 47.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 51.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | Jimbo la Kiembesamaki |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kateuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |
| 58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

**Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**BARAZA LA NANE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 12 Juni, 2013**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

**DUA**

*Mhe. Spika,(Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya na leo hii kukutana tena katika mkutano huu muhimu, mkutano ambao ni maalum kwa ajili ya bajeti ya nchi yetu.

Kama ilivyokawaida ninayo taarifa niwape waheshimiwa wajumbe kuhusiana na kazi ambayo tumeifanya kwenye mikutano ya huko nyuma. Waheshimiwa wajumbe katika Mkutano wa Kumi wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 16/01/2013 hadi tarehe 29/01/2013 Baraza lilipitisha Miswada minne ya Sheria kama ifuatavyo:-

1) Mswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini Nam 5 mwaka 2006, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

2) Mswada wa Sheria wa Kuanzishwa Shirika la Utangazaji Zanzibar, Kazi, Majukumu na Utawala wake, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

3) Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Shirika la Meli Zanzibar, Kazi, Uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

4) Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa wajumbe kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 90(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012. Naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa wajumbe hiyo ndiyo taarifa na nakushukuruni sana kwa kukupeni taarifa hiyo, ahsanteni sana.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyeke, kuanzia tarehe 20 April 2013. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kny (Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo):** Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo , naomba kuwasilisha hotuba ya Mipango ya Maendeleo na makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka 2013, 2014. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa wajumbe tunairekebisha orodha wetu wa shughuli za leo kuna kiongozi mmoja mzito tulimsahau. Kwa hiyo naona sasa kwa marekebisho hayo nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti, wa Wenye viti ili nae kuwasilisha Hati Mezani.

**Mhe. Salmin Awadh Kny(Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti):** Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenye Viti naomba kuwasilisha Hati Mezani juu ya hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenye viti juu ya mpango wa makadirio na mapato ya matumizi na kazi za kawaida kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2013/2014. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 140

### Tishio la Amani Nchini.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu linalohusu uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar, naomba uniruhusu kusema machache Mhe. Spika na kwa heshma ya hali ya juu.

Kwanza kabla ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kama nilivyotangulia kusema kwa kipindi cha miezi miwili tuliacha hapa na kurudi tena tukiwa hai, ingawa sisi ni maiti watarajiwa wakati wowote, huu sio uwezo wetu wala nguvu zetu.

Mhe. Spika, nitakuwa sijakufanyia haki wewe mwenyewe Mhe. Spika, kama sikushukuru kwa jinsi ya Baraza hivi unavyoliendesha kwa hekima zako, uwezo wako na kwa ufundi. Hapa siku zote Mhe. Ismail Jussa anasema sijui mrithi wako atakuwa nani pindipo ukiacha kazi hii. Mwenyezi Mungu akupe afya njema, akulinde na maadui na akupe umri mrefu.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa nataka niwapongeze wananchi wa Zanzibar pamoja na Tanzania Bara kwa jumla kwa kutumia haki yao ya kikatiba vizuri kwa kutoa maoni ya Katiba mpya ya Jamuhuri ya Muungano katika mazingira ya amani na utulivu. Imani yangu kuwa hatua hiyo itaendelea katika ngazi ya pili na Baraza la Katiba kabla ya Bunge la Katiba kujadili rasimu ya katiba na wananchi wake kupewa nafasi ya mwisho yakupiga kura ya maoni.

Waheshimiwa Wajumbe hapa naomba kidogo tuwe makini, tukaweka maslahi ya nchi mbele kuliko ya kisiasa. Hayo ndio maoni yangu, baada ya maelezo hayo naomba swali langu Nam. 140 linalohusu uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar lipatiwe jawabu.

Mwezi wa April mwaka huu Jeshi la Polisi nchini limesema kuna tishio la ugaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania.

(a) Je SMZ imechukua hatua gani za tahadhari ya kukabiliana na matukio kama hayo.

(b) Kwa kuwa Zanzibar tegemeo lake kubwa kiuchumi ni sekta ya Utalii hatua gani zimechukuliwa za kuimarisha doria katika maeneo ya fukwe kwa kutumia boti maalum.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Alijibu:-

Mhe. Spika, nami kabla ya kujibu swali tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha tena hapa leo katika Baraza lako hili tukufu na kutuwezesha kufanya yale ambayo tumeyakusudia. Nawaombea Wajumbe wetu wa Baraza hili na wananchi wetu wa Zanzibar ili tufanye shughuli zetu kwa amani, utulivu, umoja na upendo. Kwa maelezo haya naomba Mwenyezi Mungu atusaidie.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 140 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, mnamo mwezi wa Aprili 2013 baada ya Jeshi la Polisi kupokea taarifa za tishio la ugaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania. Vikosi vyetu vya ulinzi na usalama vilichukua hatua zote za tahathari za kiulinzi pamoja na kuanzisha operesheni katika sehemu zote zilizotiliwa mashaka. Aidha Kamati za ulinzi na usalama za Mikoa na Wilaya zilikaa kujadili tishio hilo, na elimu ya Polisi jamii ilitolewa katika vijiji vyote vilivyo kando kando ya bahari ya hindi.

b) Mhe. Spika, kwa kuelewa kuwa tegemeo kubwa la kiuchumi la Zanzíbar ni utalii, hatua kadhaa zimechukuliwa kwa kuimarisha doria katika fukwe zetu, na maeneo ya bahari.

Aidha jeshi la polisi kwa kushirikiana na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar na wananchi wanaendelea na wajibu wa kulinda raia na mali zao, katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, yakiwemo maeneo ya fukwe na baharini kwa kutumia vyombo mbali mbali vya kukabiliana na uhalifu ikiwemo boti.

Hata hivyo ujenzi wa vituo hivyo vya Polisi katika maeneo ya fukwe umeanza yakiwemo maeneo ya Kiwengwa, Fumba, Nungwi na kadhalika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri. Kilio kikubwa cha jeshi la polisi ni uhaba wa mafuta hasa katika kanda za doria za pwani.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kusaidia kuwapatia mafuta katika doria hizo.

(b) Kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia je, serikali imechukua hatua gani ya kulijenga uwezo jeshi la polisi baada ya kutumia njia za kubahatisha kama anavyobahatisha kukamata kwake baadhi ya watu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, jeshi la polisi kwa mujibu wa katiba linahudumiwa na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pale panapotokea matatizo mbali mbali kwa kuwa linafanya kazi zake pia na Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar husaidia kwa kiasi fulani jeshi hilo ili liweze kumudu kutenda kazi zake vizuri ikiwemo kuwasaidia mafuta pale wanapokuwa na upungufu.

Aidha jeshi la polisi limeanzisha mpango wa maboresho katika jeshi la polisi, ni na madhumuni ni kulisaidia jeshi kuwa na uweledi, kwa maana ya kuwa na taaluma, kuwa na vitendea kazi vya kisasa, kuwa na makaazi bora na kufanya kazi kwa kufuata wajibu wa kipolisi. Kwa hiyo hatua hizo zinaendelea na zinachukuliwa ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mhe. Mansoor Yussuf Himidi:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri nina swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri, tunaelewa kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiongozwa na dokta Shein, imeweka será na mkakati wa utalii kwa wote kutokana na umuhimu wa sekta hiyo ya utalii. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na serikali na jeshi la polisi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina vikosi vyake vyenyewe vilivyoasisiwa mwaka 1964, kwa kulinda mamlaka ya Zanzibar, uhuru na usalama wa raia na mali zake.

Je, serikali haioni umuhimu katika kulinda sekta hii ya utalii na watalii wenyewe kuruhusu askari wa vikosi hivi kufanya doria na hatimae kufanya ulinzi kwenye mahoteli haya, na wenye mahoteli wapo tayari hata kuwalipa askari hao.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, ni kweli suala la utalii ni uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar. Na ni kweli kuhakikisha kwamba ulinsi na usalama katika sekta hii unaimarishwa ili tuwe na utalii endelevu.

Mhe. Spika, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona umuhimu wa kuwa na kikosi maalum kinachosimamia ulinzi katika mambo ya utalii. Hivi sasa mipango inafanywa ili vikosi vyetu hivi kushirikishwa kikamilifu katika kupambana na uhalifu katika ukanda mzima wa utalii.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Zanzibar wengi wao hawaelewi suala hili la ugaidi, hususan vijijini na kwa kuwa suala hili hivi sasa linajitokeza mara kwa mara katika nchi yetu. Je, Mhe. Waziri utachukua hatua gani za kuwaelimisha wananchi hawa ili wakae na tahadhari na kulielewa suala hili la ugaidi yatakapotokea madhara ili waweze kujikinga. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, ni wajibu wa jeshi la polisi katika kuhakikisha linalinda usalama wa raia na mali zao kutoa taaluma mbali mbali zile ambazo zinaashiria uhalifu kwa nia ya kudhibiti uhalifu huo. Tunaupokea ushauri wako na tutawasiliana na jeshi la polisi ili ichukue hatua ya kutoa taaluma ya kila aina ya uhalifu ikiwemo suala zima la ugaidi ambalo linaweza kutokea mahali popote pale ulimwenguni.

**Nam. 32**

**Uanzishaji wa "Sober House"**

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir -** Aliuliza:-
Hivi karibuni tumeshuhudia kasi ya kuongezeka kwa nyumba za kusaidia watu walioathirika na pombe na dawa za kulevya *(Sober House)* hata hivyo taarifa za hivi karibuni juu ya baadhi ya nyumba hizi na madai yanayosikika ya mwenendo wa baadhi ya watu wanaoziendesha zinatia mashaka kama kweli watu wanaozisimamia wanataka kusaidia kuwarekebisha vijana wetu waliopotea njia.

(a) Ni utaratibu gani ambao unatumika kuanzisha *sober house.*

(b) Je, serikali ina mipango gani ambayo ni bora zaidi ya kuziendesha nyumba hizi na kuondoa malalamiko yanayosikika mara kwa mara.

(c) Serikali inafanyaje kwa vijana ambao wamepona kuona kwamba wanapotoka *'sober houses'* wanasaidiwa ili kuanza maisha ya kawaida katika jamii na kuhakikisha kwamba hawarejei tena katika vitendo viovu vya utumiaji wa madawa yakulevya.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, napenda kuungana na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba kumekuwa na ongezeko la nyumba za marekebisho ya tabia kwa vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya maarufu kwa jina la

*Sober Houses.* Nyumba ya kwanza ilianzishwa mwaka 2009 na hadi kufikia (12) kumi na mbili hivi sasa. Harakati hizo naamini zimesaidia kwa kiasi kikubwa kuwaondoa vijana katika matumizi ya dawa hizo na naamini wengi wetu ni mashahidi wa hilo.

Utaratibu unaotumika kwa wanaotaka kuanzisha huduma hiyo hupaswa kuwasiliana na kupitia Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa madhumuni ya kupata ushauri wa kitaalamu na muungozo juu ya uendeshaji wa huduma hiyo ambayo msingi wake mkuu ni programu ya upatikanaji nafuu inayojulikana kwa lugha ya kigeni kama *ROSC (Recovery Oriented System of Care.* Hivyo tume imeshirikiana na wato hudma kuhakikisha kwamba huduma inayotolewa ni sahihi na hakuna mambo yanayokwenda kinyume na programu hiyo au maadili yetu.

(b) Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitis Tume ya kuratibu na udhibiti wa madara ya kule imechukua kila juhudi kuona kwamba nyumba hizo zinakuwa chachu ya kufanikisha lengo lililokusudiwa na sio vyenginevyo. Muongozo rasmi wa uanzishwaji na uendelezaji wa nyumba hizo umetayarishwa na unategemewa kuwasilishwa kwa wahusika mara tu matayarisho yote yatakapo kamilika. Muongozo huo pamoja na mambo mengine unaweka kipa umbele kwamba huduma za programu za kuwacha dawa za kulevya zinatekelezwa katika mazingira yatakayozingatia usalama na afya bora kwa wapataji nafuu hao.

Vigezo vya uwanzishwaji na masharti ya kuzingatiwa katika sobar house vimeainishwa ikiwa ni pamoja na kwamba wanaozisimamia nyumba hizo kuwa ni weledi wa programu ya ROSC. Muongozo huu utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kukabiliana na malalamiko yanayosikika mara kwa mara. Hata hivyo tume ya kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya umekuwa na utaratibu maalum wa kuzitembelea na kufanya mikutano na vipindi maalum na wahusika wa nyumba hizo katika kujadili changamoto mbali mbali zinazojitokeza.

Natoa wito kwa kamati za shehia katika maeneo husika kuwa karibu na taasisi hizo na kuziona kwamba ni mkombozi katika kujenga vijana imara watakaosaidia katika ujenzi wa taifa letu.

(c) Mhe. Spika, ni kweli vijana wanaotoka katika *Sober House* wanahitaji kujengewa mustakbali mwema ili waweze kurejea katika maisha ya kawaida ndani ya jamii na kujiepusha na vitendo viovu. Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika suala linalofanana na hili

katika vikao vilivyopita, Ofisi yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kupitia program ya kazi nje nje, imewapatia mafunzo ya ujasiri amali imewapatia vijana 58 kutoka katika *Sober House* za Bububu, Nyarugusu, Uzi Meli Nne na *Zanzibar Youth Forum.* Aidha jumla ya vijana walipatiwa 25 walipatiwa mafunzo ya awali ya kompyuta na kuhitimu katika *Zanzibar Youth Forum* ya Canada.

Mhe. Spika, Taasisi ya Umoja wa mataifa ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) yenye Ofisi yake ya Kanda Nairobi nchini kenya kupitia programu yake inajulikana kwa jina la *sustainable livelihood* imeonesha nia ya kusaidia mradi wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa *Sober House* ya Limbani Kisiwani Pemba. Kimsingi makubaliano kati ya Ofisi yetu na Taasisi ya UNODC juu ya programu hiyo yamefikiwa. Naiomba jamii kutokuwatenga na kuwapa kila msaada vijana walioachana na matumizi ya madawa ya kulevya ili waweze kuchangia katika maendeleo ya jamii yetu.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri yanatosheleza nilikuwa nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa vijana hawa wakati wakitumia madawa ya kulevya hupoteza imani yao ya dini, na kipindi cha nyuma kulikuwa na utaratibu wa kuwapeleka vijana hawa katika Markarz ili kurudisha zile imani zao za dini. Ni sababu gani zilizopelekea utaratibu huu kutokuwepo tena hivi sasa.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Ahsante sana Mhe. Spika, nikweli kwamba kulikuwepo na programu za aina hiyo ndani ya *sober houses* zetu na bado zinaendelea. Inawezekana tu kwa sasa hawaondoshwi Zanzibar kwenda katika maeneo yaliyo mbali ya Zanzibar, lakini shughuli nzima za kuzingatia maadili ya dini kwa vijana wanaowacha dawa katika *sober houses* hizo kwa dini zote wanazingatia na kuna muda maalum wa kufanya mafunzo hayo na watu ambao wanautaalamu wa dini, mashekhe na ambao wana utaalamu wa dini nyengine wanakaribishwa katika *sober houses* hizo katika vipindi tofauti kuwasaidia vijana hao ili kuwarudisha katika imani zao.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na wizara yake kwa kuwasaidia vijana hawa waliyokuwepo *sober houses* kila pale anapopata nafasi kiuwezo.

Mhe. Spika, kwa kuwa waanzilishi wa *Sober Houses* ni watu binafsi na hawana uwezo mkubwa wa kutosha. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba ipo haja ya serikali kutoa fungu maalum kwa kila mwezi kwa vijana hawa wa *sober houses* ili waweze kujikidhi haja.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais**: Mhe. Spika, ni kweli kwamba *Sober Houses* zimeanzishwa kwa jitihada za watu binafsi na sisi tunaunga mkono jitihada hizo kama serikali. Mhe. Spika, nia na madhumuni ya serikali ni kuweza kuzisaidia sana *Sober Houses* hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Itakumbukwa kwamba kuanzia bajeti ya mwaka jana na ya mwaka huu ambayo tunamaliza nayo tulianza kutenga fedha ingawaje sio kubwa sana kutokana na uchache wa bajeti yenyewe, kila *Sober House* tuliweza kuipatia shilingi milioni moja na laki tano ili kusaidia katika harakati zao.

Vile vile kwa kujua umuhimu wa taasisi hii serikali yenyewe inampango wa muda mrefu wa kuanzisha nyumba yake ya kurekebisha tabia, nimekuwa naeleza hapa kwamba tayari tunachokiwanja katika eneo la Tunguu na mchoro wa kujenga jengo lenyewe upo tayari na serikali katika mwaka huu ilitegemea kutuingizia shilingi milioni mia moja katika kuanza harakati za kujenga kituo hicho, kwa bahati mbaya hadi kufikia mwezi Mei hatukupata pesa kutokana na bajeti kukatwa kutokana na ununuzi wa meli. Lakini katika bajeti hii tunategemea kwamba tutaingiziwa fedha ili kuanza harakati za serikali yenyewe kujenga kituo chake.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ninakushukuru Mhe. Spika, naomba niulize swali dogo tu la nyongeza kwa Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mheshimiwa katika majibu yake ameelezea jinsi ya jitihada zinazofanya serikali katika kuongeza masuala ya *Sober House* na amesisitiza viongozi kushirikiana na masheha basi kuona umuhimu wa kuendeleza hilo suala la *Sober House*. Swali langu Mheshimiwa lipo hapa, je, haoni kama hilo ni tatizo la kuanza kushajihisha masuala ya kuendeleza *Sober House* na ni sababu ya kuweza vijana kuona kwamba hata wakitumia madawa ya kulevya serikali inawajali na kuwasaidia.. Nilitaka kujua labda wizara yake imejenga mikakati gani kuhakikisha kwamba hawa watumiaji wa madawa ya kulevya wanamalizika kabisa na serikali iachane na mpango wa kuwatengenezea mazingira baada ya kutumia madawa ya kulevya.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, tatizo la vijana wanaotumia madawa ya kulevya katika visiwa vyetu ni kubwa sana na *research* ambazo zilifanyika miaka ya nyuma zinatwambia kwamba kuna watu ambao wameathirika hasa vijana katika matumizi ya dawa za

kulevya wasiopungua 8,000 hizo ni *research* za zamani lakini Ofisi yetu inafanya utafiti kujua hali ikoje kwa hivi sasa.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuzuia vijana wetu wasiingie katika matumizi ya dawa za kulevya, Tume ya kuratibu udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya inafanya jitihada za makusudi katika kutoa elimu, kwanza katika kutoa elimu na kufika katika sehemu mbali mbali katika vijiwe vya vijana katika maskuli na katika maeneo ambayo vijana wanapatikana ili kuwapa elimu juu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya kwa lengo la kuwazuia vijana wasiathirike na matumizi ya dawa za kulevya.

Nia na madhumuni ya serikali ya kuzisaidia *Sober Houses* haipo katika kuendeleza kwamba vijana watumie ili wende pale warekebishwe tabia. Mhe. Spika, tayari taifa lina vijana hawa ambao wameathirika na ni watoto wetu na upo utaratibu ambao vijana hawa wanaweza kugeuzwa kuacha tabia yao hii wakarudi katika jamii na wakawa vijana bora. Nia na madhumuni ya serikali kusaidia jitihada hii ni kuwaokoa wale ambao tayari wameshaathirika katika matumizi ya dawa za kulevya ili kuwageuza tabia zao.

**Nam. 13**

**Ujenzi wa Mabanda Bora ya Kuuzia Vyakula**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-**

Akinamama wa Zanzibar wameitikia wito wa Serikali kujiajiri katika kupambana na umasikini lakini bado wanafanya kazi katika mazingira magumu kutokana na maeneo yao ya biashara kuwa machafu kama mabanda ya vyakula katika soko kuu la Darajani na mabanda ya chakula soko la samaki Malindi.

(a) Serikali ina mpango gani wa kujenga mabanda ya kisasa ambayo yatawavutia watu wengi na kuongeza kipato badala mazingira yanayotumika hivi sasa.

(b) Kwa kuwa suala la usafi ni muhimu kwa biashara ya chakula, kwa nini Serikali inaachia bidhaa za vyakula kufanyika katika mazingira machafu na ya kutisha.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Alijibu:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 13 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua na inathamini sana juhudi zinazofanywa na kinamama mbali mbali katika

kujiajiri wenyewe. Tunawapongeza wale wote wenye mtazamo wa kujitegeme na kupunguza umaskini wa kipato. Mhe. Spika, katika kuweka mazingira bora ya kuunga mkono jitihada hizo, Baraza la Manispaa itajenga banda la kisasa kwa ajili ya wafanyabiashara ya chakula (mama lishe) katika Soko la Darajani na jengine katika Soko la Mwanakwerekwe katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kumalizika kwa mabanda hayo kutaimarisha hali ya usafi kwa walaji na watumiaji wa huduma. Mheshimiwa naomba kusisitiza kwamba kujenga banda jipya si suluhu ya kuondoa uchafu, muhimu sote tubadilike katika mienendo yetu, sote tukerwe na uchafu katika mazingira yetu hasa ya chakula na majumbani mwetu.

b) Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limekuwa likichukua hatua mbali mbali kwa mujibu wa sheria katika kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hawa wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanya biashara na wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wa kuzingatia usafi wa jamii na mazingira. Aidha, kwa wale wanaokaidi hatua za kisheria huchukuliwa dhidi yao. Jumla ya kesi 189 za kufanya biashara katika maeneo machafu na yasiyoruhusiwa zimefunguliwa katika mahakama ya Mwanzo ya Malindi kati ya Septemba 2012 na Februari 2013.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Spika, Mhe.Waziri uzoefu unaonesha yanapojengwa mabanda wahusika hasa au walengwa hawanufaiki, mfano hai katika Soko la Darajani yamejengwa maduka wahusika wengine walengwa hawakupata. Je unawahakikishia vipi kinamama hawa ili kuwatoa wasiwasi kama watapata sehemu hiyo.

Pili, umetaja mahkama wananchi wamekosa amani sana na mahkama ya Baraza la Mji uliyoitaja hapo Malindi kwa kutokutendewa haki, je unachukua hatua gani kuwaelimisha wahusika katika kesi hizo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, niseme kwamba tunajitahidi kwa kiwango kikubwa hapa tunazungumzia yale maduka au mikahawa ya mama lishe sio maduka, lakini kwa faida yake nasema kwamba tutajitahidi hata hayo maduka ambayo kama kwa makosa basi waliopewa sio waliovunjiwa basi tutafanya *review* tutayapitia tuone kwamba kama wamekosa pale wapatiwe pengine. Lakini tutajitahidi tuone kwamba kweli waliyoondolewa pale wanarudishwa pale au pengine.

Suala la mahakama sasa hilo Mheshimiwa mimi niseme nitajitahidi kutoa elimu tu kwa watu wetu hatuwezi kuingilia huo ni muhimili mwengine wa mahkama, wao wana kazi zao. Sasa kama wao wanatoa maamuzi ambayo si sahihi mimi siwezi kusema lakini ninachotaka kusema, muhimu tuwaelimishe watu wetu wafate taratibu na taratibu za kufanya biashara mle mnamohusika kwa mujibu wa sheria tulizoziweka wenyewe.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa majibu ya Mhe. Waziri anasema serikali iko katika mpango wa kutafuta maeneo na kuweza kuyaweka maeneo ya wafanyabiashara kwa utulivu na kuwaandalia mazingira mazuri. Mhe. Waziri hivi karibuni tutakumbuka kinamama wauzaji samaki mbele ya soko la samaki tuliwapiga sana virungu, je, Mhe. Waziri huoni iko haja hivi sasa kwa kuwa serikali inajitayarisha kuwaachia wale kinamama wakafanya biashara zao ili na wao waondokane na umaskini na iwe ni sera ya serikali ili kuwaondoshea umaskini kinamama.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba ni nia yetu kuwasaidia na kuwajengea uwezo kinamama na wananchi wengine waweze kujitegemea na kupunguza makali ya maisha. Lakini tunachosisitiza, wafanye hayo kwa mujibu wa taratibu na sheria ziliopo, tusifanye mambo kienyeji, hatuwezi kuchukua sinia za samaki tukapanga pembeni mwa barabara kwanza hatari ya usalama wao, pia uchafu na kuharibu mazingira. Wewe mwenyewe Mhe. Mshimba siku zote unatushauri tuweke mji safi. Sasa matumbo yale wanatumbua samaki pale, wanapara wanatupa kiholela, hakuna mji unaoendeshwa hivyo. Sasa lazima tufanye kazi tupange mji twende kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa, mji wetu uwe safi.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. spika, ninakushukuru sana na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kwanza Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Waziri atuelimishe ni mara ngapi kama Waziri ametembelea soko la samaki Darajani na Malindi ili kuona hali ilivyo.

(b) Mhe. Waziri amesema kwamba wale ambao wanapinga sheria kwa kufanya biashara katika maeneo machafu na maeneo yasiyoruhusika, hupelekwa mahkamani na kiasi ya kesi 189 ziko mahkamani. Ni kwa nini sheria ipo na serikali imeweka mahakama kwa ajili ya kuwahukumu watu lakini vikosi vya manispaa huchukua biashara za wafanyabiashara hawa, kuzila na kuziharibu na kuwapiga, wakati mahkama ipo kwa ajili ya kutoa haki kwa wale wanaofanya makosa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:**

**(a)** Mhe. Spika, Mhe. Hija na mimi ni mnunuzi wa samaki wa Darajani na Malindi kwa hivyo pale sipishi siku mbili, tatu na mimi ninafika. Pia katika moja ya kazi yangu nakwenda katika wakati wowote kuona mambo yanakwenda vipi, nakwenda kienyeji tu siendi kama Waziri. Lakini kwa kweli hao tunaowazungumza wanauza samaki nje, bila ya taratibu wanafanya baada ya saa za kazi, kuanzia saa tisa pale na visinia vyao wanakaa nje mpaka jumba refu kule.

(b) Askari wetu wa Baraza la Manispaa tumechukua juhudi tumewaelimisha, tumewafahamisha, lakini bado kwa kweli tuseme wanafanya ukaidi. Sasa hatupendi mapambano, hatupendi malumbano, huyu wa Mhe. Hija huyu wa Mhe. Mwinyihaji tunawaelimisha na wao wachukue jukumu lao la kufata sheria na taratibu za nchi. Sasa ningekuomba sana Mhe. Hija tusaidiane kama mwakilishi. Ninajua unao marafiki zako, unao unaowaweza pale tuwaelimishe wafate tu wafate sheria. Na ikiwa kuna haja ya kujenga sehemu nyengine ya kwenda wao kuuza samaki basi tutajenga hivyo. Lakini tusikhalifu sheria kwa kutaka useme unataka nipate kipato sivyo hivyo, tusishindane na serikali.

**Nam. 38**

**Jumuiya za Kiraia katika Kusaidia Jamii**

**Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:**
Jumuiya za kiraia zina mchango mkubwa sana katika suala la uwajibikaji wa utoaji huduma kwa wananchi na jamii *(Social Accountability Monitoring)* lakini hakuna fungu maalum la bajeti kwa jumuiya hizo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani katika kufikiria kuweka sheria ya kuanzisha fungu au mfuko maalum katika kuzijengea uwezo jumuiya za Kiraia.

(b) Je, Serikali ina thamini kwa kiasi gani mchango wa jumuiya za kiraia katika kutowa huduma kwa jamii.

**Mhe Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 38 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, Jumuiya za Kiraia ni Jumuiya zinazotakiwa kuanzishwa kisheria chini ya sheria namba 6 ya mwaka 1995 kwa lengo la kusukuma na kuharakisha maendeleo hasa katika maeneo ambayo Serikali haijafikia

kikamilifu. Kwa mfano, AGAKHAN FOUNDATION, ZANZIBAR STUDENTS WELFARE na kadhalika.

Msingi mkuu wa kuanzishwa Jumuiya za kiraia unatokana na fikra na mtazamo wa wanzilishi wa jumuiya juu ya matatizo ya kijamii ambayo wanahisi wakiungana wanaweza kuyatatua kwa kutumia ama rasilimali walizonazo zikiwemo fedha, zana na vitendea kazi, nguvu kazi na hata utaalamu walionao. Mara nyingi jumuiya hulazimika kutafuta rasilimali zinazohitajika kutoka vyanzo mbali mbali nje ya wanajumuiya, kwa mfano: Wahisani, Mashirika na Jumuiya za Kimataifa hata watu binafsi ili kutekeleza shughuli na malengo yake kwa mujibu wa katiba na sheria inayoongoza jumuiya hiyo.

Jukumu la Serikali ni kuhakikisha kwamba Jumuiya za kiraia zinafanya kazi zao kisheria pamoja na kuzijengea uwezo hasa wa kitaalamu katika undeshaji wa shughuli za jumuiya husika. Serikali imekuwa ikilitekeleza jukumu hilo kuptia taasisi zake kwa kuzingatia aina ya kazi zinazotekelezwa na jumuiya hiyo. Kwa nfano, jumuiya zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI kama ZAPHA+ zinapata mchango mkubwa kutoka Kamisheni ya UKIMWI.

Pia Wizara ya Afya kwa mfano imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa na Jumuiya ya Zanzibar Outreach Program katika kutoa matibabu katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Aidha Jumuiya ya *Z help* nayo imefanikiwa kufanya ukarabati mkubwa katika Skuli ya Unguja Ukuu kwa mashirikiano makubwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Pamoja na hayo Serikali imeweza kuziongezea nguvu na uwezo kiutendaji jumuiya za kiraia. Aidha Serikali imetowa misamaha ya kodi kwa jumuiya kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa jumuiya kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji jumuiya na kuongeza uwezo wao wa utekelezaji wa malengo yao. Aidha serikali inaendelea na kazi ya kuifanyia marekebisho sheria ya jumuiya za kiraia ili kuhakikisha inakwenda na wakati tulionao.

Serikali kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na kwa kushirikiana na Idara yangu ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Usajili wa Biashara na Mali imekuwa ikiandaa vikao maalum na jumuiya za kiraia ili kutathmini utendaji, uwajibikaji, changamoto zinazozikabili jumuiya za kiraia na mchango wa jumuiya za kiraia katika ulekelezaji wa maendeleo yao. Aidha Wizara yangu imeanzisha kitengo maalum cha kuratibu shughuli za jumuiya za kiraia utaratibu na muongozo waliojipangia kisheria. Aidha taasisi mbali mbali za serikali zimejiwekea utaratibu wa kushirikiana na taasisi za kiraia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya jumuiya hizo.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kumuuliza Waziri suala dogo la nyongeza. Mhe. spika, kama Waziri alivyoelezea katika kulijibu suala langu kuwa jumuiya hizi za kiraia ziko kisheria. Je, kwa sababu wananchi wetu wanaojipanga kujipatia riziki kwa jumuiya hizi ambazo si za kiserikali je, kuna mpango gani kuweza kujifanyia alau sherehe na kutoa zawadi japo siku moja ndani ya mwaka mzima, ili kuzipa kipa umbele kuwa na changamoto kubwa wafanyakazi.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo Jumuiya za Kiraia ni jumuiya zilizoanzishwa kwa lengo maalum na wananchi wenyewe kwa kusaidia kitu fulani. Sasa sisi serikali, wizara yangu inaratibu utekelezaji wao kutokana na katiba yao walivyofanya. Na uratutibu huo ndio utatulazimisha sisi kuanzisha kitengo maalum cha ukaguzi, ukaguzi huo tunapitia kila jumuiya kutizama kama kweli yale malengo ambayo yamo katika katiba yao ndivyo wanavyofanya na hapo tunawafahamisha, tunawarekebisha na hata wakati mwengine tunawapatia wataalam.

Sasa kuhusiana kwamba tutafanya sherehe maalum za kila mwaka kuwapa jumuiya fulani hilo bado hatujafanya kwa sababu lazima tujiandae, tuwe na kifungu maalum. Sasa si shauri baya ni shauri ambalo tutalifanyia kazi kama ikiwezekana tunaweza tukafanya na kama haitowezekana tunaweza tukaambizana.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri amekiri hapa amesema kuwa serikali inashirikiana na jumuiya hizi kwa mambo manne mbali mbali ameyataka. Lakini Mheshimiwa sasa hivi wakati wa bajeti je, Wizara yake imetenga kiasi gani ya kuwasaidia jumuiya hizi.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo Wizara yangu haijatenga kiasi kadha cha kuwasaidia jumuiya hizi. Wizara yangu imetenga fedha katika kitengo cha ukaguzi ambacho kina lengo la kuzikagua hizi jumuiya na kuwaelekeza ni mambo gani na mambo gani je yanakwenda kwa mujibu taratibu za kisheria au hayendi, hapo ndio tunaweza tukawaelekeza wafanye nini na nini kuendeleza jumuiya zao. Kwa hivyo fedha zitakazokuwepo katika bajeti yangu ni fedha za kitengo cha ukaguzi wa Jumuiya.

**Nam. 91**

**Kupatikana Soko la Uhakika kwa Wakulima wa Mwani**

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad – Aliuliza:**
Kwa kuwa akinamama wa Kaskazini Pemba wakiwemo vijiji vya Tumbe, Shumba ya Mjini, Kwale, Micheweni, Maziwa ng'ombe n.k wakiendesha maisha yao kutegemea kilimo cha mwani na kwa kuwa katika siku za karibuni soko la mwani halikuwa la uhakika jambo ambalo lilipelekea usumbufu mkubwa wa maisha ya wakulima wa zao hili, ambao huuza mwani siku mbili kwa mwezi.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Je, kama Serikali inajua hilo ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali katika kuwapatia soko la uhakika wananchi wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:**

Mhe. Spika naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 91 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inalijua suala hili.

(b) Kwa kuelewa ukubwa wa tatizo na umuhimu wa kilimo cha mwani kwa maisha ya wananchi wanaojishughlisha na kilimo hicho, Wizara ilifanya ziara katika nchi zinazosafirisha mwani kama Zanzíbar kwa dhamira ya kubadilishana uzoefu katika masoko ya zao hilo na kuona ni namna gani tutaweza kuinua maslahi ya wananchi wanaojishughulisha na kilimo hicho. Mhe. Spika, Napenda kutumia nafasi hii kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba tatizo hili linaathiri wakulima wengi wa kilimo hiki duniani kutokana na wigo mdogo wa soko la bidhaa hiyo. Ili tuweze kuinarisha maslahi ya wakulima ambao wanatumia nguvu na muda mwingi kwa tija na maslahi madogo tunapaswa kuchukua hatua za kusarifu mwani hapa hapa Zanzíbar ili kuongezea thamani na hatimae tuweze kuuza bidhaa za zao hilo kuliko tunavyofanya hivi sasa. Mwelekeo wa Wizara ya Biahsara, Viwanda na Masoko kwa mwaka ujao ni kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kufanya utafiti kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kulisarifu zao la mwani kulifalia soko lake pamoja na bidhaa zake.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Ahsante Mhe. spika, ninamshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyaeleza. Lakini tatizo hili limekuwa ni tatizo la siku nyingi na bado linaendelea kuwepo na kwa kuwa wananchi hawajengi matumaini mazuri ya kuwa serikali inawafatilia suala hili

na tatizo hili linalowakabili. Sasa je, Mhe. waziri unawaambiaje wananchi wakulima wapandaji wa mwani katika suala hilil na kunajitokeza mawakala wanaonunua mwani katika bei tofauti wengine 300 wengine 400. Je Mhe. Waziri utawaelezaji wananchi ili wapati matumaini na serikali yao kuondokana na tatizo hili.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Spika, tumesema kwamba serikali tunalifahamu hilo tatizo lakini tukumbuke kwamba zao la mwani biashara yake ilipitishwa kwenye sheria kwamba iingie katika *private sector* sio serikali lakini ni biashara inayofanywa na wafanyabiashara binafsi. Lakini pamoja na hayo kwa sababu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni katika kutoa huduma basi tumeona ni vyema tushirikiane na Wizara kama nilivyosema ya uvuvi na mifugo ili kulifanya utafiti zao hili kwa lengo zuri tu Mhe. Spika, la kusaidia wafanyabiashara hawa wazalishaji wa zao la mwani, ili na wao waweae kupata bei nzuri katika soko la bidhaa za mwani.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kuuliza swali la nyongeza kuhusu mwani. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini kwa kuwa wananchi wetu wameitikia wito wa kilimo cha mwani kwa wingi sana kwa ajili ya kujisaidia katika kukimu maisha yao na kwa kuwa waziri amekiri kama wanatafuta soko wamepita katika maeneo yanayonunua mwani ili kubadilishana mawazo na kuona kama wananchi wanapata soko. Lakini kwa kuwa Wizara hii ya biashara pamoja na kuwa sio wanaonunua mwani ni sekta ambayo ni ya watu binafsi, lakini wao kama wasimamizi wakuu kwa sababu serikali ndio inakuwa msimamizi mkuu hata kwa zile sekta binafsi. Na kwa kuwa Wizara ya Biashara ndio inayosimamia suala hili huko kwa watu binafsi. Je, haioni kama kuna haja ya kukutana na hao wanunuzi wa mwani na wakawaeleza wananchi hasa bei halisi iliyoko na wakawaeleza sababu za msingi za kuwa mwani unakaa mara nyingi haununuliwi ili wananchi wakawa wanajua kuliko kunyamaza kimya na ikiwa wananchi wakawa wanapata habari za pale na pale tu.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Ahsante Mhe. Spika, kupata nafasi hii na mimi kujibu swali la Mhe. Subeit ni kweli kwamba bei ya mwani ina matatizo lakini nataka nimfahamishe sana Mhe. Spika, kwamba suala la mwani linashughulikiwa na Wizara mbili, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tunashughulikia suala la bei, yaani masoko ya mwani na uzalishaji au upandaji unashughulikia na Wizara Uvuvi na Mifugo. Kwa hivyo naomba asichanganye madawa la kwanza.

Lakini la pili kiasi miezi mitatu iliyopita yaani mwani ilikuwa kabisa hauna soko yaani wale wanauza mwani ilikuwa kabisa mwani haunununuliwi na wananchi wengi walikuwa na mwani umekaa katika nyumba zao kwa muda mrefu bila ya kununuliwa, ambayo hii ni hasara kubwa sana. Hasara moja kwa mwani ule kama haukununuliwa kwamba mwani sio bidhaa kama karafuu au bidhaa nyengine. Mwani unapokaa katika nyumba ya mtu kwa muda wa miezi 4 bila kununuliwa unaanza kupungua viini vyake vya ubora. Kwa hivyo Wizara ya Biarashara imefanya kazi kubwa ya kuangalia namna gani ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu kwanza mwani wao ununuliwe na pili uwe unanunuliwa kwa bei nzuri.

Mimi mwenyewe nimeshiriki katika mkutano wa mwani duniani uliofanyika Indonesia mwezi uliopita na nimekutana na wenye viwanda wengi, nimekutana na wanunuzi wa viwanda wengi na kwa kweli katika suala hili kuna utata mmoja uliojitokeza kwamba uzalishaji wa mwani duniani umezidi sana viwango vya mahitaji ya mwani; yaani mwani duniani ni mwingi kuliko matumizi, matumizi yako pale pale lakini uzalishaji wa mwani umekuwa mkubwa sana. Hiyo ndio iliyofanya bei ya mwani kushuka duniani. Kwa hivyo katika masomo ya mwani duniani bei ya mwani imeshuka sana ukilinganisha na miaka ya nyuma. kwa hivyo, hivi hili hasa ndio lililofanya wafanyabiashara wa mwani Zanzibar wakasita kununuwa mwani ilikuwa hawanunui mwani kabisa kabisa. Kwa hivyo Zanzibar, tunatoa mwani karibu tani elfu kumi na tano kwa mwaka na hizo tani elfu kumi zinatoka kisiwani Pemba, tani elfu nne zinatoka Zanzibar, na tani elfu moja zinatoka Tanzania Bara. Kwa jumla tani elfu kumi na tano zinatoka Zanzibar. Na katika Afrika ni nchi ya mwanzo inayotoa mwani mwingi kupeleka nje.

Kwa bahati mbaya mwani tunaozalisha ni mwani wa aina *spinosium* yaani ni bei ya chini kuliko mwani mwengine unaouzwa duniani. Kwa hivyo ni kweli bei ya mwani imeshuka. Mimi mwenyewe nimekwenda Pemba nimekaa kwa muda wa wiki moja na nimewatembelea wakulima wa mwani na wanunuzi wa mwani; tumekubaliana na wanunuzi wa mwani kwa sasa hivi wanunue mwani kwa bei hiyo waliyokubaliana kutokana na masomo yao, bei hiyo inayouzwa kwa bei ya shilingi mia nne kwa sababu masoko ya Marekani yanaruhusu kuuzwa kwa shilingi mia nne na wengine wananunua kwa shilingi mia tatu kwa sababu masomo yao ya Europe ni shilingi mia tatu. Kwa hivyo ninawaambia wafanyabiashara ya mwani waendelee na ukulima wa mwani na wauze kwa bei itayokuwa sasa hivi, ipo tamaa kwa siku za mbele bei ya mwani kupanda kidogo. Lakini kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri pale tunafanya mikakati ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuweza kuutumia mwani katika kufanya viwanda hivyo ili tuuze bidhaa na tuziuze mali ghafi.

kwa hivyo muda huu ninawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watusaidie Wizara ya Biashara kuwaelimisha wananchi kwamba bei ya mwani imeshuka lakini kilimo cha mwani wasikiache, bei itapopanda tutakuwa tumekula hasara. Kama ilivyo karafuu, karafuu sisi tulikuwa tumekodisha tani nyingi zaidi, karibu tani elfu kumi na nne, kumi na mbili hadi kumi na nane. Mikarafuu tumeikata sasa hivi tunatoa tani elfu nne, wenzetu Madagascar wanatoa tani elfu kumi na mbili. kwa hivyo kilimo cha mwani tukikiwacha bei ya mwani itakapopanda itakuwa ni hasara kubwa kwa Zanzibar, tujitahidi kulima mwani na sisi Serikali tutajitahidi kutafuta masoko ya mwani ili wapate bei nzuri.

**Mhe. Asha Bakari Makame**: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha katika kipindi hichi na ninamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tupitishe bajeti zetu za kila wizara kwa salama na amani.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana na ya kirefu sana, tatizo kubwa Mhe. Spika, Waziri atueleze tatizo gani?, sisi tunasema soko. Ni tatizo gani ambalo linatatiza mwani huu kutokupata soko. Pili kwa sababu mwananchi anapovuna mwani wake anatakiwa na yeye angalau apate chochote, lakini leo Mhe. Waziri, ameeleza mwenyewe kwanza ukiuweka miezi miwili au mitatu basi hamna kitu. Je, namuomba Mhe. Waziri, Mhe. Spika, tuhakikishe ni tatizo gani la soko ambalo linamfanya mpanda mwani kuwa hapati soko, ni tatizo gani?

**Mhe. Waziri wa Biashara na Masoko**: Mhe. Spika, ninaomba nirejee tena kwamba uzalishaji wa mwani duniani umezidi mahitaji, ndio ikabidi bei ya mwani duniani iteremke. Kwa hivyo inapofika wakati ikawa uzalishaji unapunguwa ndio bei ya mwani inapanda. Sasa la kufanya hapa nchini kwetu huu mwani tuule, tuule wenyewe tuanze utamaduni wa kula mwani, wenzetu mwani wanakula na sisi tuanzishe viwanda vidogo vidogo na tuule mwani, hata biriani unaweza kupikia. Ahsante Mhe. Spika.

## KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

**Mhe. Spika**: Nafasi ya maswali imekwisha haidhuru muda upo. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais**: Mhe. Spika, kwa kuwa leo ni siku ya kuwasilisha Bajeti ya Serikali, na kwa mujibu wa kanuni 23(1) vikao vya Baraza vinatakiwa kuanza taa 3.00 asubuhi na kuendelea hadi saa 7.00 mchana, na kuendelea tena saa 11.00 jioni mpaka saa 1.45 usiku. lakini kwa kuwa tuna utamaduni wa kuahirisha kikao chetu tunapokuwa

tunakusudia kusoma Bajeti ya Serikali ili kusoma Bajeti hiyo jioni saa 10.00 ili kutoa nafasi vizuri kwa waziri anaesimamia mambo ya fedha aweze kuwasilisha vyema Bajeti ya Serikali. Basi kwa sababu hiyo Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu chini ya kanuni 23(2) uakhirishe kikao hichi mapema kabla ya saa 7.00 ili tuweze kurudia tena saa 10.00 jioni kwa ajili ya hotuba ya Bajeti ya Serikali. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** waheshimiwa wajumbe hoja imetolewa, wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa hoja, waliokubali wameshinda. Makofi)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 4.09 Asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 10:00 jioni)*

*(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2013/2014

### TAARIFA YA SPIKA

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tunao utamaduni kwamba siku ya bajeti kama leo Waziri anayehusiana na masuala ya fedha huwa amejificha pahala na baadae ataingia pale tutakapomwita rasmi. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kwanza kuwakaribisha wageni wetu ambao wamefika na kushirikiana nasi katika shughuli hizi tutawatambua baadae, lakini shughuli yetu ya leo ni Mkutano wa Bajeti na punde tu hivi tunategemea kumuomba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuingia ndani hapa ukumbini na hatimaye tutawatambua rasmi wageni wetu waliokwishafika. Lakini wakati huu naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye anasindikizwa na wajumbe wawili wazito kuingia humu ndani, naona wanamleta pale.

Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri ambaye sasa anaingia ndani ya ukumbi. Mhe. Waziri karibu sana uwasilishe Hotuba ya Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:** Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako tukufu likae kama Kamati maalum ya kujadili na hatimae kuidhinisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2013/14. Ombi hili linalenga kutimiza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kama ilivyorekebishwa. Kama ilivyo desturi, sambamba na Hotuba hii, naomba pia kuwasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi mwaka 2012 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2012/13 kama yanavyoonekana katika Kitabu cha Kwanza. Aidha, katika Kitabu cha Pili nawasilisha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/14 na mwisho ni rasimu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2013/14. Naomba maelezo hayo nayo yawekwe katika kumbukumbu za Baraza.

Mhe. Spika, tumekutana tena hapa kuzungumzia mipango muhimu ya maendeleo ya nchi yetu na watu wake, Wazanzibari. Naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba kwa kutubariki uwezo huu wa kujumuika tena leo hii. Namuomba atujaalie hekima katika kukiendesha kikao hiki muhimu na tumalize kikao tukiwa tumewatumikia vyema, kwa busara na kwa ukweli Wananchi wenzetu tunaowawakilisha.

Mhe. Spika, tumeshuhudia kipindi chengine cha juhudi kubwa kwa Mhe. Rais wetu na wasaidizi wake katika kutuletea maendeleo. Tumeshuhudia pia kuimarika kwa amani na utulivu nchini petu, pamoja na matukio machache yaliyoashiria kuharibu utulivu wetu, hatua za haraka za kuyadhibiti matukio hayo zilizochukuliwa na serikali yetu imeweza kurejesha hali ya nchi kuwa ya shwari. Kifungu cha 26 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinatamka kwamba Rais ndie “Mkuu wa Nchi ya Zanzibar, Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi”. Hatua za maendeleo na utulivu tunazozishuhudia, kwa hivyo, ni matokeo ya uongozi huo wa Mheshimiwa Rais. Naomba basi nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliojaa hekima, busara na kuona mbali. Kwangu binafsi, namshukuru pia kwa kuendelea kuniamini na kunipa jukumu la kuiongoza Ofisi yake hii muhimu inayoshughulikia Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, nimesema kuwa tulikuwa na matukio machache ya kuharibu utulivu katika kipindi hiki. Miongoni mwa matukio hayo ya kusikitisha na kutia huzuni ni yale ya kushambuliwa na kuathiriwa kwa viongozi tofauti wa dini na Sheha. Kwanza, Sheikh Fadhil Soraga, aliemwagiwa tindikali mapema ya asubuhi ya tarehe 6 Novemba 2012. Likafuatia tukio la kupigwa risasi kwa Mchungaji Amros Mkenda asubuhi ya tarehe 25 Disemba mwaka 2012.

Mwenyezi Mungu muumba alituonesha uwezo wake, akamlinda na kwa rehema zake bado Padri Mkenda yuko hai. Tukio kubwa zaidi ni lile lililotokea asubuhi ya tarehe 17 Februari mwaka huu kwa kupigwa risasi na kuuwawa kwa Mchungaji Everest Mushi. Tukio la karibuni kabisa ni la kumwagiwa tindikali Sheha wa Shehia ya Tomondo, Bw. Mohammed Said Kidevu lililotokea tarehe 23 Mei mwaka huu.

Mhe. Spika, kwa vyovyote vile matukio yote hayo yalilenga kuwadhuru kwa kiasi kikubwa viongozi wetu hawa wa dini zetu kubwa na shehia; yalilenga kuleta fitna kubwa katika jamii yetu kwa kugombanisha waumini wa dini tofauti; na hatimae yalilenga kuleta fujo nchini na kuondoa utulivu uliozoeleka. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuepusha na shari zote za matukio hayo na kutuepusha na makusudio ya wahusika. Nawashukuru na kuwapongeza sana wananchi wote, na hasa ndugu, jamaa na wafuasi wa karibu wa viongozi wote hao. Nawashukuru na kuwapongeza kwa utulivu wao na imani yao kwa serikali katika kipindi chote cha majaribu.

Mhe. Spika, wakati Serikali bado inaendelea na jitihada za kuwapeleka wahusika katika mikono ya sheria, tuendelee wote kunasihiana katika kudumisha utulivu tuliouonesha wakati wachache wetu walipotutia majaribuni. Kwa Sheikh Soraga, Mchungaji Mkenda na Sheha Mohammed Kidevu tunawaombea kwa Muumba muweza awaponyeshe haraka na kuwaondolea khofu ya matukio yao. Kwa Mchungaji Mushi tunamuombea malazi mema na kwa ndugu, marafiki na waumini wake tunawaombea subira zaidi. Hakika Mwenyezi Mungu atalipa kwao kwa subira yao na hataacha kuwalipa waliotenda uovu huo kwa dhulma yao kwa viongozi hao wote wasio na hatia.

Mhe. Spika, naamini uongozi mzuri wa Mhe. Rais umesaidiwa pia na utendaji na ushauri anaoupata kutoka kwa wasaidizi wake wakuu, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais. Naomba nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati Makamo hao wa Rais kwa uongozi wao.

Mhe. Spika, kipindi kama hiki mwaka jana, wananchi wenzetu wa Jimbo la Bububu hawakuwa na Mwakilishi katika Baraza hili kufuatia kifo cha aliekuwa Mwakilishi wao, Ndugu Salum Amour Mtondoo. Kupitia uchaguzi mdogo, tayari pengo hilo limezibwa na limezibwa vyema. Nawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kuchagua Mwakilishi wao na mimi nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) kwa kuchaguliwa kuliwakilisha Jimbo hilo humu Barazani. Naamini kwa utendaji aliouonesha Mhe. Hussein tokea kuchaguliwa kwake, wananchi hao

wameridhika na chaguo lao. Namtakia kila la kheri Mhe. Hussein katika kuwatumikia na kuwawakilisha vyema wananchi wa Jimbo la Bububu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niwasilishe Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2012 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2012/13 hadi kufikia Machi 2013.

# MAPITIO YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI KWA MWAKA 2012/13

## Hali ya Uchumi Duniani na Kikanda

Mhe. Spika, uchumi wa dunia unaendelea kukua taratibu kutokana na matatizo ya kiuchumi na fedha yaliozikumba nchi za Ulaya. Uchumi wa dunia mwaka 2012 umekuwa kwa wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2011. Kanda zote nazo zimeshuhudia kasi ndogo ya kukua kwa uchumi wake kwa mwaka 2012 kama hivi ifuatavyo:

(i) Uchumi wa nchi zilizoendelea umekuwa kwa wastani wa asilimia 1.2 kutoka asilimia 1.6 mwaka 2011;
(ii) Uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi umekuwa kwa wastani wa asilimia 5.1 kutoka asilimia 6.1 ya mwaka 2011;
(iii) Uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara umekua kwa wastani wa asilimia 4.8 kutoka asilimia 5.3 mwaka 2011; na
(iv) Katika Afrika ya Mashariki ukuaji ulifikia wastani wa asilimia 4.5 kutoka asilima 5.9 mwaka 2011.

## MFUMKO WA BEI WA DUNIA, AFRIKA NA KANDA

Mhe. Spika, tofauti na ukuaji wa uchumi, mwenendo wa utulivu wa bei za bidhaa na huduma Duniani na katika Kanda zote umekuwa wa kuridhisha kwa mwaka 2012, kwa kupungua kasi ya wastani wa mfumko wa bei, kama inavyobainishwa hapo chini:

(i) Kasi ya mfumko wa bei duniani imepungua kutoka asilimia 3.8 mwaka 2011 kufikia 3.3 mwaka 2012;
(ii) Kwa nchi zilizoendelea ilishuka na kufikia asilimia 1.3 mwaka 2012 kutoka asilimia 1.4 mwaka 2011;

(iii) Kwa nchi zinazoibuka kiuchumi na zinazoendelea zilishuka kutoka asilimia 7.2 mwaka 2011 na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2012; na

(iv) Nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara mfumko wa bei ulipungua hadi asilimia 9.1 mwaka 2012 kutoka asilimia 9.3 mwaka 2011.

(v) Kwa nchi za Afrika ya Mashariki, ulishuka kutoka asilimia 13.2 mwaka 2011 hadi kufikia wastani wa asilimia 11.5 mwaka 2012.

## MWENENDO WA UCHUMI WA ZANZIBAR

### Pato la Taifa

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar umeonesha mwenendo mzuri tofauti na ule wa Dunia na Kanda. Ukuaji halisi wa uchumi umeimarika zaidi mwaka 2012 na kufikia asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.7 wa mwaka 2011. Pato la Taifa kwa bei za miaka husika limefikia jumla ya Shilingi 1,354 bilioni mwaka 2012 ikilinganishwa na Shilingi 1,198 bilioni kwa mwaka 2011.

Miongoni mwa mambo yaliyochangia ukuaji huo ni pamoja na haya yafuatayo:

(i) Ongezeko la ukuzaji rasilimali kwa asilimia 41.3 kutoka thamani ya Shilingi 183.20 bilioni mwaka 2011 hadi kufikia Shilingi 258.87 bilioni. Ongezeko hili limesababishwa na uwekezaji mkubwa katika maeneo ya ujenzi wa nyumba za kuishi na biashara, zana za usafirishaji na ujenzi vijijini.

(ii) Ukuaji mzuri wa sekta ya viwanda ambayo imekua kwa asilimia 9.2 mwaka 2012 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2011.

(iii) Kuimarika kwa sekta ya huduma ambayo imekua kwa asilimia 8.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.6 mwaka 2011.

### Pato la Mtu Binafsi

Mhe. Spika, kwa kuzingatia kiasi hicho cha Pato la Taifa na idadi ya watu milioni moja na laki tatu wa Zanzibar, kwa wastani pato la kila mtu limeongezeka mwaka 2012 na kufikia Shilingi 1,003,000/= (US$ 638) kwa mwaka kutoka Shilingi 960,000/= (US$ 617) kwa mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 4.5.

## UKUAJI NA MICHANGO YA KISEKTA KATIKA PATO LA TAIFA

Mhe. Spika, kiujumla, sekta zote zimeonesha ukuaji katika mwaka 2012 ingawa kwa viwango tofauti na kwa kasi tofauti ikilinganishwa na mwaka 2011. Viwango hivyo vya ukuaji kwa mwaka 2012 ni kama hivi ifuatavyo:

(i) Sekta ya Huduma ilikuwa kwa asilimia 8.7 ikionesha kuimarika kidogo kutoka asilimia 8.6 mwaka 2011;
(ii) Sekta ya Kilimo ilikuwa kwa asilimia 1.3 na hivyo kasi yake imeshuka kutoka asilimia 2.7 ya mwaka 2011; na
(iii) Ukuaji wa Sekta ya Viwanda ulifikia asilimia 9.2 kutoka asilimia 5.8 ya mwaka 2011, ukichangiwa zaidi na kuimarika kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za kuishi na za biashara.

Mhe. Spika, kwa upande wa mchango ya sekta hizi katika Pato la Taifa, mchango wa Sekta ya Huduma umeimarika zaidi na kufikia asilimia 45.3 kutoka asilimia 44.0 mwaka 2011. Matokeo ya kuimarika huko ni kushusha michango ya sekta nyengine. Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 30.2 kutoka asilimia 32.2 mwaka 2011, wakati sekta ya Viwanda imechangia asilimia 11.7 mwaka 2012 kutoka mchango wa asilimia 12.0 mwaka 2011.

## MFUMKO WA BEI ZANZIBAR

Mhe. Spika, mwenendo wa bei Zanzibar umeshabihiana na ule wa dunia na Kanda kwa mwaka 2012. Kasi ya mfumko wa bei ilipungua hadi kufikia asilimia 9.4 na hivyo kuwa juu kidogo kuliko matarajio ya kufikia asilimia 8.7. Hata hivyo, bado kasi hii ni chini ya kiwango cha wastani wa nchi za Afrika ya Mashariki. Kufikiwa kiwango cha tarakimu moja ni hatua nzuri ikilinganishwa na kiwango cha Mfumko wa Bei cha asilimia 14.7 kwa mwaka 2011. Kwa kuwa sehemu kubwa ya Mfumko wa Bei Zanzibar inachangiwa na uingizaji bidhaa, kasi nafuu ya Mfumko wa Bei imechangiwa na utulivu wa bei katika nchi tunazofanya nazo biashara, mwenendo mzuri wa bei za chakula na mafuta ya Petroli katika soko la dunia na utulivu wa thamani ya sarafu ya Tanzania kulinganisha na Dola ya Marekani.

## SEKTA YA NJE

Mhe. Spika, mizani ya Biashara inaonesha kuwa nakisi katika urari wa biashara imeendelea kupanuka zaidi mwaka 2012 na kufikia Shilingi 203.9 bilioni kutoka nakisi ya Shilingi 102.9 bilioni ya mwaka 2011. Hali hii imechangiwa na kasi kubwa ya kukua kwa uingizaji ikilinganishwa na ukuaji wa usafirishaji bidhaa nje. Katika mwaka huo, uingizaji ulikua kwa asilimia

65.2 kutoka Shilingi 164.2 bilioni mwaka 2011 hadi Shilingi 271.3 bilioni mwaka 2012. Kwa upande mwengine, katika kipindi hicho usafirishaji ulikuwa kwa asilimia 10 tu kutoka Shilingi 61.3 bilioni hadi kufikia Shilingi 67.4 bilioni. Hali hii imetokana na kasi kubwa zaidi ya uingizaji wa vifaa vya chuma kama nondo, mashine na vifaa vya umeme.

## UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI 2012/13

Mhe. Spika, Baraza lako liliidhinisha Bajeti ya Shilingi 648.9 bilioni kwa mwaka wa fedha 2012/13, zikihusisha Shilingi 315.8 bilioni kutokana na mapato ya ndani yatokanayo na kodi, mapato yasiyo ya kodi na mikopo ya ndani. Kiasi kilichobakia cha Shilingi 333.1 bilioni ni kutokana na Washirika wa Maendeleo, ikiwemo kwa ajili ya Programu na Miradi na Misaada ya Kibajeti. Kwa upande wa matumizi, jumla ya Shilingi 307.8 bilioni ziliidhinishwa kwa kazi za kawaida na Shilingi 341.1 bilioni kwa ajili ya Programu na Miradi ya Maendeleo.

### Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13 serikali ilikadiria kukusanya mapato kutokana na vyanzo vya ndani ya Shilingi 294.13 bilioni sawa na asilimia 21.3 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya Shilingi 274.13 bilioni kutokana na vyanzo vya kodi na Shilingi 20.00 bilioni ni kutokana na vyanzo visivyokuwa vya kodi. Kati ya Shilingi 274.13 bilioni zilizotokana na kodi, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ilitarajiwa kukusanya kiasi cha Shilingi 146.00 bilioni. Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilikadiriwa kukusanya Shilingi 106.73 bilioni na Shilingi 21.4 bilioni zilikadiriwa kukusanywa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kutokana na Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2012 hadi Machi mwaka 2013), Serikali ilikadiria kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi 224.24 bilioni. Makusanyo halisi yalifikia Shilingi 201.24 bilioni sawa na asilimia 90 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya makusanyo hayo, mapato kutokana na kodi yalifikia Shilingi 192.41 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 91 ya makadirio wakati mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia Shilingi 8.83 bilioni sawa na asilimia 69 ya makadirio ya kipindi hicho. Yakilinganishwa na makusanyo halisi ya Shilingi 169.6 bilioni ya kipindi kama hicho mwaka uliopita (2011/12), kunajitokeza ukuaji wa mapato ya Shilingi 31.6 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 18.7. Ukusanyaji mapato kitaasisi na kwa kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka uliopita ni kama hivi ifuatavyo:

(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya jumla ya Shilingi 79.51 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio. Ukusanyaji huu unamaanisha ukuaji wa mapato wa asilimia 18.5 kutoka Shilingi 67.1 bilioni;

(ii) Bodi ya Mapato Zanzibar imekusanya jumla ya Shilingi 109.48 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio zikiwemo Shilingi 100.65 bilioni za mapato ya kodi sawa na asilimia 87 ya makadirio na jumla ya Shilingi 8.8 bilioni zilitokana na mapato ya mawizara. Mapato ya *ZRB* yamekuwa kwa asilimia 15.6 kutoka Shilingi 94.7 bilioni za mwaka uliopita;

(iii) Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imekusanya Shilingi 12.3 bilioni kutokana na Kodi ya Mapato (*PAYE*) kwa wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania waliopo Zanzibar ambayo ni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya kipindi hicho.

Mhe. Spika, matarajio ya sasa ni kukusanya Shilingi 269.6 bilioni kutokana na mapato ya ndani hadi kufikia Juni 2013, sawa asilimia 91 ya makadirio ya mwaka huo. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia Shilingi 258.3 bilioni sawa na asilimia 94 ya makadirio, wakati mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia Shilingi 11.33 bilioni, sawa na asilimia 57 ya makadirio. *TRA* inatarajiwa kukusanya jumla ya Shilingi 105.51 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio. Kwa upande wake, *ZRB* inatarajiwa kukusanya jumla ya Shilingi 142.68 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 86 ya makadirio na mapato ya *PAYE* ni Shilingi 21.4 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio.

**Mapato ya Nje**

Mhe. Spika, kati ya Shilingi 333.2 bilioni zilizotarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, jumla ya Shilingi 196.3 bilioni zimepatikana hadi kufikia Machi 2013, zikiwa ni pungufu ikilinganishwa na Shilingi 199.05 bilioni zilizopatikana hadi kufikia Machi 2012. Kati ya fedha hizo, Shilingi 175.8 bilioni ni ruzuku na mikopo kwa ajili ya Program/Miradi ya Maendeleo ambayo kimsingi haikuongezeka sana kutoka Shilingi 174.95 bilioni za mwaka 2011/12. Misaada ya kibajeti imeshuka hadi kufikia Shilingi 20.5 bilioni mwaka 2012/13 kutoka Shilingi 24.1 bilioni mwaka 2011/12 ambazo ni pungufu kwa asilimia 17.5. Hali hii imesababishwa na kukwama kwa sababu za kiutendaji, kwa sehemu ya Zanzibar ya misaada inayopitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**DENI LA TAIFA**

Mhe. Spika, Deni la Taifa hadi mwezi wa Machi, 2013 limefikia Shilingi 252.3 bilioni sawa na asilimia 18.6 ya Pato la Taifa. Deni hili ni sawa na ongezeko la asilimia 20 kutoka deni la Shilingi 209.9 bilioni lililoripotiwa katika mwezi wa Machi 2012. Kati ya deni hilo, deni la ndani ni Shilingi 48.5 bilioni na lile la nje ni Shilingi 203.8 bilioni (US$ 128.1 milioni). Kati ya deni la ndani, Shilingi 3.1 bilioni ni deni la Kiinua Mgongo baada ya kulipa jumla ya Shilingi 5.8 bilioni kwa wastaafu 617. Matarajio kwa kipindi cha miezi mitatu iliyobaki ni kuwa deni hili litafikia jumla ya Shilingi 3.5 bilioni kwa wafanyakazi watakaostaafu mwezi wa Aprili hadi Juni 2013.

**MATUMIZI**

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, serikali ilitarajia kutumia jumla ya Shilingi 648.3 bilioni kwa mwaka unaoendelea wa fedha. Kwa miezi tisa matumizi yote yalitarajiwa kufikia Shilingi 434.1 bilioni. Katika kipindi cha tathmini, matumizi halisi yamefikia jumla ya Shilingi 428.0 bilioni sawa na asilimia 98.6 ya makadirio ya miezi tisa au asilimia 66 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa matumizi ya fedha za ndani, jumla ya Shilingi 231.67 bilioni sawa na asilimia 93 ya makadirio ya miezi tisa zimetumika. Kati ya matumizi hayo Shilingi 205.79 bilioni ni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 97 ya makadirio ya Shilingi 212.34 bilioni na Shilingi 25.88 bilioni ni mchango wa serikali katika kazi za maendeleo, sawa na asilimia 71 ya lengo la miezi tisa. Kiasi kilichobakia cha Shilingi 196.3 bilioni kimetokana na fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2012/2013**

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/13 ulilenga kutekeleza jumla ya programu 38 na miradi 84 ya maendeleo kupitia klasta tatu zinazounda MKUZA II ambapo programu sita na miradi 18 ni mipya. Jumla ya Shilingi 341.1 bilioni zilitengwa kwa madhumuni hayo. Kati ya fedha hizo Shilingi 47.9 bilioni sawa na asilimia 14 ni kutoka serikalini na Shilingi 293.2 bilioni sawa na asilimia 86 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Katika kipindi cha utekelezaji cha Julai - Machi 2012/13, jumla ya Shilingi 201.69 bilioni zimetumika kugharamia utekelezaji wa Programu/Miradi ya Maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 59 ya bajeti yote ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilinhi 25.88 bilioni ni mchango wa serikali sawa na asilimia 54 ya makadirio ya mwaka ya mchango wa serikali na Shilingi 175.81 bilioni ni

mchango wa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 60 ya makadirio ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa upande wa utekelezaji ki-Klasta, Klasta ya kwanza ya Ukuzaji Uchumi na Upunguzaji Umaskini wa Kipato ilitekeleza jumla ya programu 21 na miradi 25 yenye makisio ya jumla ya Shilingi 197.9 bilioni sawa na asilimia 58 ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2012/13. Fedha zilizotolewa kwa kipindi cha miezi tisa cha Julai-Machi ni Shilingi 136.8 bilioni sawa na asilimia 69 ya bajeti ya Klasta. Kati ya fedha hizo, serikali imechangia Shilingi 8.2 bilioni sawa na asilimia 43.4 ya fedha iliyojipangia na Washirika wa Maendeleo walichangia Shilingi 128.6 bilioni sawa na asilimia 71.8 ya fedha zilizopangwa. Miongoni mwa Miradi mikubwa iliyokamilika chini ya Klasta hii ni ule wa uwekaji wa njia mpya ya umeme kutoka chini ya Bahari uliofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la Changamoto za Milenia (*MCC*). Kwa mara nyengine tena kwa niaba ya serikali na watu wa Zanzibar, nawashukuru sana watu wa Marekani na Serikali yao kwa msaada huu adhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, Klasta ya pili ya Huduma za Ustawi wa Jamii ilitekeleza jumla ya programu 11na miradi 33 iliyokadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 117.7 bilioni sawa na asilimia 35 ya bajeti ya maendeleo katika mwaka 2012/13. Fedha zilizotolewa kwa kipindi cha miezi tisa ni shilingi 50.9 bilioni sawa na asilimia 43 ya bajeti ya Klasta. Kati ya fedha hizo, Serikali imechangia shilingi 5.85 bilioni sawa na asilimia 42.7 ya fedha iliyojipangia na Washirika wa Maendeleo walichangia shilingi 45.07 bilioni sawa na asilimia 43.3 ya fedha zilizopangwa.

Mhe. Spika, Klasta ya tatu ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa ilitekeleza jumla ya programu sita na miradi 26 yenye jumla ya shilingi 25.42 bilioni sawa na asilimia 7.4 ya bajeti ya maendeleo katika mwaka 2012/13. Fedha zilizotolewa kwa kipindi cha miezi tisa cha Julai - Machi ni shilingi 13.97 bilioni sawa na asilimia 54.9 ya bajeti ya Klasta. Kati ya kiasi hicho, Serikali imechangia shilingi 11.82 bilioni sawa na asilimia 77.2 ya fedha iliyojipangia na Washirika wa Maendeleo walichangia shilingi 2.14 bilioni sawa na asilimia 21.2 ya fedha zilizopangwa.

## UTEKELEZAJI MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2012/13

Mhe. Spika, Serikali ilibainisha maeneo mbali mbali ya kipaumbele katika katika Bajeti yake ya mwaka 2012/13. Maeneo hayo ni pamoja na Kuimarisha huduma za afya; Kuimarisha ajira kwa vijana; Kuimarisha ustawi wa wazee; Kuimarisha elimu ya lazima; Kuimarisha uchumi; na Kuimarisha mashirikiano ya Sekta Binafsi na Umma. Tumeendelea kupiga hatua katika

kuyafikia malengo yetu. Hata hivyo, utekelezaji umefikia viwango tofauti baina ya Sekta. Maelezo kamili ya hatua iliyofikiwa kwa kila eneo yatatolewa na Waheshimiwa Mawaziri husika katika hotuba zao za bajeti.

## SENSA YA WATU NA MAKAAZI

Mhe. Spika, itakumbukwa kuwa nchi yetu ilifanya Sensa ya Watu na Makaazi katika mwezi wa Agosti mwaka 2012. Serikali ilifanya jitihada maalum kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa Sensa. Matokeo ya Sensa hii yalitangazwa rasmi na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 31/12/2012. Matokeo hayo yameonesha kuwa nchi yetu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa ina jumla ya wakaazi 44,928,923. Sensa pia imebainisha kuwa idadi yetu katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba imefikia watu 1,303,569 ambapo watu 896,721, sawa na asilimia 69, wanaishi Unguja na watu 406,868, sawa na asilimia 31 ya watu wote wa Zanzibar, wanaishi katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, matokeo haya ya Sensa pia yanaashiria kuwa idadi ya watu Zanzibar imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 2.8 kwa mwaka tokea Sensa ya mwaka 2002. Pamoja na kupungua kwa kasi yetu ya ukuaji wa idadi ya watu kutoka asilimia 3.1 kwa mwaka baina ya Sensa zilizopita, bado kiwango hiki cha asilimia 2.8 ni kikubwa na jitihada zaidi zinahitajika ili kukidhibiti. Kwa upande mwengine, Sensa pia imebainisha changamoto nyengine muhimu ambayo ni mkusanyiko mkubwa wa watu katika miji yetu. Kwa mujibu wa takwimu za Sensa, karibu nusu ya Wazanzibari wote, yaani asilimia 46, sawa na watu 593,678, wanaishi katika Mkoa wa Mjini/Magharibi. Kwa kuzingatia ukubwa wa Mkoa wenyewe, idadi hiyo ya wakaazi inafanya wakaazi wa kila kilomita moja ya mraba kwa mkoa huu kuwa ni watu 2,581 ambayo ni ya pili kwa ukubwa kwa Tanzania ikitanguliwa na Dar Es Salaam yenye wastani wa wakaazi 3,133 kwa Kilomita ya Mraba. Uchambuzi muhimu wa takwimu za Sensa unaendelea na matokeo yake yataendelea kutolewa kwa awamu.

## MAANDALIZI YA KATIBA MPYA YA JAMHURI YA MUUNGANO

Mhe. Spika**,** katika hotuba yangu ya mwaka jana nilizungumzia pia mchakato wa uandaaji wa Katiba mpya ya Jamhuri yetu ya Muungano na kuwanasihi wananchi wote kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani. Niliwaomba kustahamiliana pale tunapokuwa na mitazamo inayotofautiana. Nawashukuru wananchi walio wengi kwa kuisikiliza Serikali na kuwa watulivu. Hata hivyo,

sio wote waliokuwa na busara na hekma ya ustahamilivu. Wakati kwa ujumla mchakato wa ukusanyaji wa maoni juu ya Katiba hiyo umekwenda vizuri, kulijitokeza matukio yasiyopendeza na ya kuhatarisha amani. Tunashukuru hali imetulia kwa sasa lakini lazima tutumie uzoefu wa mchakato huo kujifunza. Tunahitaji kukuza demokrasia yetu kwa ustaarabu wa kuruhusu misimamo na mitazamo tofauti miongoni mwetu. Mchakato wenyewe wa kuipata hiyo Katiba mpya unaendelea. Mafunzo tuliyoyapata katika hatua ya ukusanyaji wa maoni yatuongoze vyema katika hatua zitakazofuata hadi kukamilika kwake.

Mhe. Spika**,** tayari Tume ya Mabadiliko ya Katiba imeshatoa Rasimu ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna hatua nyengine kadhaa hadi kupatikana kwa Katiba mpya kama zilivyooneshwa katika Sheria ya Tume hiyo. Ni wajibu wa kila mmoja wetu na sote kwa pamoja kuhakikisha kwamba mageuzi haya muhimu katika nchi yetu hayatufarakanishi, sio wenyewe kwa wenyewe miongoni mwetu Wazanzibari wala baina yetu na ndugu zetu wa Tanzania Bara. Kwa vyovyote vile, kwa kuzingatia historia, muingiliano na ukaribu wa nchi zetu bado tunahitajiana baina yetu na Tanzania Bara. Bado tunahitaji ujirani ulio mwema na wa mashirikiano hata kama tungekuwa nchi tofauti, seuze leo tumo katika Jamhuri moja ya Muungano. Tukamilishe basi mchakato wa kupatikana Katiba mpya tukiendelea kuwa wamoja na ndugu.

Mhe. Spika, baada ya mapitio hayo ya utendaji wetu wa miezi tisa ya mwanzo ya mwaka 2012/13, naomba sasa nielezee kwa mukhtasari mwelekeo wa hali ya Uchumi kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2013/14.

## MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA MAPINDUZI

Mhe. Spika, kuwepo kwetu hapa leo na demokrasia tunayojinasibisha nayo ni matokeo ya kazi kubwa na ya kishujaa iliyofanywa na wazee wa Taifa letu ambao walijumuika na kujitolea muhanga ili kizazi chetu kiwe huru na kuweza kujiamulia wenyewe mambo yake na kujiletea maendeleo. Matokeo ya kujitolea kwao muhanga ni Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964. Tukijaaliwa, tarehe kama hiyo mwakani tutaadhimisha kutimia kwa mwaka wa 50 tokea kugombolewa kwa Zanzibar yetu. Hii ni siku adhimu na itahitaji maadhimisho yanayofanana nayo. Serikali imejipanga na kujiandaa vyema na maadhimisho hayo.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI 2013

Uchumi wa Dunia na wa Kanda

Mhe. Spika, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kufikia asilimia 3.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.2 kwa mwaka 2012. Hali hii ya ukuaji mzuri inatarajiwa pia katika kila Kanda kama ifuatavyo :

(i) Kwa nchi zilizoendelea ukuaji unatarajiwa kufikia asilimia 1.2 mwaka 2013 kama ilivyokuwa mwaka 2012.

(ii) Kwa nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.3 kwa mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2012;

(iii) Uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuimarika zaidi kwa kukua kwa asilimia 5.6 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2012.

## MFUMKO WA BEI WA DUNIA

Mhe. Spika, kasi ya mfumko wa bei duniani unatarajiwa kushuka kufikia asilimia 3.1 kwa mwaka 2013 ukilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2012. Nchi zilizoendelea, kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kupanda kufikia asilimia 4.1 kwa mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 1.3 mwaka 2012. Aidha, mfumko wa bei kwa nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi hautakuwa na mabadiliko unatarajiwa kuwa asilimia 5.9 kwa mwaka 2013 kama ilivyokuwa mwaka 2012. Hata hivyo, mfumko wa bei kwa nchi za Kusini ya Jangwa la Sahara unatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 7.2 mwaka 2013 ukilinganishwa na asilimia 9.1 mwaka 2012.

## HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013 uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kuendelea kuimarika na kukua kwa asilimia 7.5 kutoka ukuaji wa asilimia 5.0 mwaka 2012.

Matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2013 yanatokana na mambo yafuatayo:

(i) Kukamilika kwa uwekaji wa waya wa umeme wa chini ya bahari kutoka Ras Kiromoni Tanzania Bara hadi Ras Fumba.

(ii) Kuimarika kwa sekta ya utalii kutokana na kupanuka kwa wigo wa bidhaa na huduma za utalii zinazofanywa na wajasiri amali, vile vile kukuza na kutangaza utalii katika soko la ndani na nje ya nchi kwa dhana ya utalii kwa wote.

(iii) Kuendelea kuimarika kwa vyanzo vya mapato.

(iv) Utekelezaji wa program ya mapinduzi ya kilimo Zanzibar.

(v) Kuendelea kuimarika kwa mashirikiano baina ya sekta za Umma na Binafsi.

(vi) Kupatikana kwa mkongo *fiber optic* ambao utarahisisha shughuli za huduma ya mawasiliano.
(vii) Kuvutia wawekezaji katika kuimarisha maendeleo ya viwanda vidogo vidogo nchini.
(viii) Kuimarisha uvuvi wa bahari kuu na ufugaji wa mazao ya baharini.
(ix) Kuendelea kwa uwekezaji katika kuimarisha miundombinu hasa ya barabara na viwanja vya ndege.
(x) Kuendelea na jitihada za usambazaji wa umeme vijijini na visiwa vidogo vidogo.
(xi) Kuendelea kuimarika kwa amani na utulivu wa kisiasa.

**Mfumko wa Bei**

Mhe. Spika, mfumko wa bei unatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 7.9 mwaka 2013 ukilinganishwa na asilimia 9.4 mwaka 2012. Matarajio hayo ya kushuka kwa kasi ya mfumko wa bei yanatokana na:

(i) Kushuka kwa mfumko wa bei duniani;
(ii) Kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa mazao ya chakula na biashara;
(iii) Kuimarika kwa Sekta ya Uvuvi; na
(iv) Kuendelea na utulivu wa sarafu ya Tanzania.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2013/14

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/14 Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo utazingatia zaidi utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II), Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano wa MKUZA II, Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya mwaka 2015 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010.

## MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2013/14

Mhe. Spika**,** haitarajiwi kwamba vipaumbele vya Serikali viwe vinabadilika sana mwaka hadi mwaka. Mengi ya maeneo ya kipaumbele yanahitaji uwekezaji wa muda mrefu ili kufikia malengo ya maendeleo ya nchi. Tunahitaji kujenga Taifa lenye maendeleo makubwa ya kiuchumi; lenye watu walioelimika, wataalamu wa hadhi ya kimataifa na wenye siha na wasiosumbuliwa na maradhi yanayoepukika. Kwa kuzingatia ukweli huu, bado kipaumbele cha Serikali kitaendelea kuwa katika kukuza kwa kasi zaidi uchumi wetu na kuongeza ajira, hususan kwa vijana, kuimarisha ubora wa elimu, kuimarisha huduma za afya hususan katika upatikanaji wa dawa za lazima na katika upatikanaji wa maji safi na salama. Maeneo haya yote yataendelea kujitokeza kama kipaumbele kwa miaka ijayo ya fedha.

Mhe. Spika, ajira itaendelea kuimarishwa kupitia Program mbalimbali za uwekezaji kama vile katika Kilimo, Viwanda na Utalii. Jambo la msingi ni kuhakikisha uendelevu wa ukuaji wa uchumi, kwa kasi kubwa zaidi na kwamba ukuaji huo lazima utafsirike katika kuleta ajira bora. Kuhusu elimu, Sekta hii inapaswa kuwa kipaumbele cha Taifa kwa muda wote. Mafanikio makubwa tayari yamefikiwa katika usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa elimu hadi ngazi ya sekondari. Kipaumbele cha serikali katika sekta hii muhimu kitaendelea kuwa katika kuimarisha ubora wake. Kwa upande wa afya, bado upatikanaji wa dawa na visaidizi *sundries* utaendelea kupata umuhimu maalum. Kwa upande mwengine, Serikali inatambua shida wanayoipata wananchi katika maeneo mbalimbali kuhusiana na upatikanaji wa maji safi na salama. Mkazo utaendelea kuwekwa katika kuhakikisha kuwa huduma hii ya lazima kwa uhai inapatikana kwa wananchi walio wengi.

Mhe. Spika**,** mambo yote haya yatafanyika bila ya kupuuza umuhimu wa miundombinu ya msingi kama vile barabara, bandari, viwanja vya ndege, umeme ikiwemo kutafuta chanzo mbadala cha nishati hiyo, kwa maendeleo ya nchi yetu. Katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka ujao wa Fedha, Miundombinu ya Barabara, Viwanja vya ndege na Bandari imepangiwa jumla ya shilingi 62.7 bilioni, ile ya Kilimo na Ufugaji jumla ya shilingi 15.0 bilioni na ya Nishati jumla ya shilingi 9.6 bilioni.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba wakati tukiendelea na bajeti ya Serikali ya mwaka 2012/13, nilitoa kauli ya Serikali juu ya ahadi yake ya ununuzi wa meli mpya ya abiria na mizigo. Sote kwa pamoja tulikubaliana na haja ya kujibana katika matumizi, kwa kukata bajeti ya Wizara zote, ili kupatikana fedha kwa madhumuni hayo. Kwa bahati mbaya, mchakato wa kupata mjenzi wa meli hiyo umehitaji muda mrefu kukamilika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Serikali imeamua kujenga meli hiyo badala ya kununua meli iliyotumika. Aidha, kwa maumbile yake, suala hili limehitaji majadiliano ya kina ya kiufundi, kifedha na kisheria. Hata hivyo, nina furaha kulijulisha Baraza lako Tukufu kuwa hatimae mchakato huu umepiga maendeleo mazuri na tayari mkataba wa ujenzi baina ya SMZ na Kampuni ya Daewoo International ya Korea ya Kusini. Meli hiyo yenye uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na tani 200 za mizigo itagharimu Dola za Kimarekani **30.4** milioni sawa na shilingi 48.6 bilioni na inatarajiwa kujengwa kwa kipindi cha miaka miwili na kuwasili nchini mwezi Juni 2015.

Mhe. Spika**,** naomba nitaje kwa ufupi jinsi maeneo ya kipaumbele yalivyozingatiwa katika Bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo:

(i) Jumla ya shilingi 55.4 bilioni zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maji safi na salama;

(ii) Sekta ya Elimu imetengewa shilingi 32.8 bilioni;

(iii) Sekta ya Afya imetengewa jumla ya shilingi 23.9 bilioni; na

(iv) Programu ya Ajira kwa Vijana imetengewa shilingi 1.1 bilioni kwa ajili ya ajira ya moja kwa moja, zaidi ya ile inayotokana na utekelezaji wa Programu na Miradi mbalimbali kama nilivyoeleza awali.

Kwa ujumla, katika Bajeti ya mwaka ujao wa fedha, maeneo haya manne tu ya kipaumbele yametengewa jumla yashilingi 113.2 bilioni kati ya shilingi 305.4 bilioni. Kiasi hiki ni zaidi ya theluthi moja ya Bajeti yote ya Mpango wa Maendeleo, sawa na asilimia 37 ya Bajeti hiyo. Kwa kuzingatia kiasi hicho kikubwa cha uwekezaji kinachotengwa kwa ajili ya huduma hizo, bajeti ya mwaka ujao wa fedha ni Bajeti ya Huduma za Jamii kwa wananchi wa Zanzibar**.**

Mhe. Spika, sambamba na vipaumbele hivyo, maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa Dira ya 2020 na MKUZA II yamewekwa katika Programu tano kubwa kama ifuatavyo:

**A. Programu ya Mageuzi ya Kiuchumi**

Programu hii inakusudia kuziimarisha sekta ya utalii, biashara, viwanda na kilimo.

**B. Programu ya Mageuzi ya Serikali**

Programu hii ina lengo la kuimarisha Utawala Bora, Uwajibikaji na utoaji huduma kwa matokeo kwa utendaji, na utoaji huduma wa Serikali kwa kupima viashiria vya msingi vya utendaji (*KPIs*); kupambana na rushwa na kujenga uwezo.

**C. Programu ya Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu**

Kwa upande wa Kujenga Uwezo wa Rasilimali watu maeneo yatakayozingatiwa ni kuimarisha huduma za afya na ubora wa elimu.

**D. Masuala Mtambuka**

Kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi, maafa na uhifadhi wa mazingira, jinsia na watu wenye mahitaji maalum.

**E. Visaidizi (*enablers*)**

Kwa utekelezaji wa mageuzi yaliyotangulia Serikali itahitaji viwezeshaji muhimu vitakavyojumuisha uimarishaji wa miundombinu, kukuza ujuzi wa kazi na ujasiriamali, ubora na viwango na mkakati wa kuendeleza sekta binafsi.

## RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2013/14

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14 Serikali inatarajia kutekeleza jumla ya Programu 35, moja ikiwa ni mpya, na Miradi 75 ya maendeleo ambapo tisa ni mipya. Jumla ya shilingi 305.4 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kutekeleza Programu na Miradi hiyo. Kati ya fedha hizi, Serikali itatoa

shilingi 70.0 bilioni na Washirika wa Maendeleo watachangia shilingi 235.4 bilioni ikiwemo ruzuku ya shilingi 86.8 bilioni na mikopo shilingi 148.6 bilioni.

## MAANDALIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU

Mhe. Spika**,** kwa miaka miwili sasa Serikali imeendelea na matayarisho ya maandalizi ya mageuzi ya mfumo wa bajeti yenye lengo la kuimarisha uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa bajeti na unaosisitiza matokeo kutokana na matumizi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa bajeti. Mfumo huu umeanza kutekelezwa kwa majaribio mwaka huu 2012/13 na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Majaribio hayo yamehusu kutayarisha Muundo na Maelezo ya Programu yenye kuhusisha malengo, matokeo, viashiria, shabaha na gharama za Programu. Maelezo hayo yaliwasilishwa sambamba na mfumo wa sasa wa bajeti. Kwa Bajeti za mwaka ujao wa fedha wa 2013/14, wizara zote zilizobakia nazo zimeingia katika maandalizi hayo ya mfumo mpya wa Bajeti kwa kuhusisha maeneo yaliyotajwa. Matarajio ni kwamba ifikapo mwaka 2014/15 Bajeti ya Serikali iwe inaandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia mfumo huo wa Programu.

## MWELEKEO WA BAJETI 2013/14

## SURA YA BAJETI

### Mapato

Mhe. Spika**,** Serikali inatarajia kutumia jumla ya shilingi 658.5 bilioni katika mwaka wa fedha 2013/14 ikimaanisha ongezeko dogo la asilimia 1.5 kutoka Bajeti ya shilingi 648.9 bilioni mwaka 2012/13. Kwa kuzingatia uwezo wa sasa wa mapato kutokana na vyanzo vya ndani, inatarajiwa kuwa mapato ya ndani yatafikia jumla ya shilingi 333.7 bilioni na hivyo kufanya jumla ya mapato hayo kufikia shilingi 338.7 bilioni ikichanganywa na shilingi 5.0 bilioni zinazotarajiwa kusalia mwisho wa mwaka. Mapato ya ndani yanahusisha mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi, ikiwemo gawio kutoka Benki Kuu na Mashirika ya Serikali. Ikilinganishwa na matumizi yanayotarajiwa kama nilivyoyataja, kiasi hicho cha mapato cha shilingi 338.7 bilioni kitaacha nakisi ya shilingi 310.5 bilioni.

Mhe. Spika**,** katika mwaka huo wa 2013/14, Serikali inatarajia kupokea jumla ya shilingi 277.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Fedha hizi zinajumuisha shilingi 235.4 bilioni za Mikopo na Ruzuku kwa Programu na Miradi ya Maendeleo, shilingi 40.0 bilioni za Msaada wa Kibajeti na shilingi

2.5 bilioni kutokana na msamaha wa madeni (MDRI). Yakichanganywa na mapato ya ndani, jumla ya mapato yote ya Serikali inafikia shilingi 616.6 bilioni. Kwa kuzingatia matumizi yote ya Serikali ya shilingi 658.5 bilioni mapato haya yataacha nakisi ya shilingi 41.9 bilioni.

Mhe. Spika**,** ili kuziba pengo hilo la Bajeti, Serikali inakusudia kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato ya ndani kwa kurekebisha viwango vya kodi na ada za huduma mbalimbali. Kwa ujumla, hatua hizo zinatarajiwa kuingiza shilingi 16.9 bilioni, na hivyo kuzidi kupunguza pengo la bajeti na kufikia shilingi25.0 bilioni. Serikali inakusudia kukopa ndani kwa kiwango hicho cha shilingi 25 bilioni na hivyo kuleta uwiano wa mapato na matumizi katika Bajeti.

**Matumizi**

Mhe. Spika**,** kati ya matumizi ya shilingi 658.5 bilioni yanayotarajiwa kwa mwaka 2013/14, shilingi 353.1 bilioni sawa na asilimia 53.6 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 305.4 bilioni sawa na asilimia 46.4 ni kwa kazi za maendeleo. Itakumbukwa pia kuwa Serikali, kupitia kwa Mhe. Rais, iliahidi kuimarisha kipato cha Mfanyakazi kila hali ya uchumi na uwezo wa serikali inaporuhusu. Katika kutekeleza ahadi hiyo, marekebisho makubwa ya maslahi ya wafanyakazi yalifanyika kuanzia mwezi Oktoba 2011. Ahadi ya Mhe. Rais bado ipo na itaendelea kutekelezwa kama alivyoahidi. Kwa azma hiyo, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali inakusudia kuimarisha tena maslahi ya wafanyakazi. Jumla ya shilingu 17.5 bilioni zimetengwa kwa madhumuni hayo na kuimarisha maslahi ya wafanyakazi pamoja na kuhudumia ajira mpya na marekebisho mengine muhimu. Kwa kutambua mchango mkubwa wa Baraza lako, marekebisho pia yamefanywa kwa maslahi ya Wajumbe wako ambao nao wana majukumu mengi.

Mhe. Spika**,** matumizi yaliyotajwa hapo juu ya shilingi 658.5 bilioni ni jumla tu ya matumizi yote. Matumizi haya yanahusisha pia yale ya lazima, kwa mujibu wa Sheria, na mengine ambayo tayari Serikali yetu ilikwishajifunga na hivyo ni lazima yafanyike. Miongoni mwa matumizi ya lazima *Mandatory Expenditure* ni haya yafuatayo:

(i) Mishahara pamoja na ruzuku shilingi 176.3 bilioni.
(ii) Malipo ya Kiinua Mgongo na Pencheni shilingi 20.6 bilioni.
(iii) Malipo ya Dhamana za Hazina na Hati Fungani shilingi 14.5 bilioni
(iv) Huduma za Viongozi wakuu, Hospitali na chakula cha shilingi 11.5 bilioni.
(v) Mchango wa Washirika wa Maendeleo kwa Programu na Miradi ya Maendeleo shilingi 235.4 bilioni.

(vi) Mchango wa SMZ kwa Programu na Miradi ya Maendeleo inayoendelea na ambayo ina mikataba yenye thamani shilingi 56.0 bilioni.

(vii) Mahitaji ya dawa, vifaa vidogo vidogo *sundries* pamoja na dawa za maabara zenye thamani ya shilingi 2.1 bilioni.

Mhe. Spika**,** kwa ujumla, kiasi cha shilingi 516.4 bilioni tayari zina matumizi maalum na haziwezi kugawanywa. Hali hii inabakisha shilingi 142.1 bilioni ambazo ndio zimegawanywa kwa ajili ya kazi za kawaida kwa Serikali na taasisi zake zinazopokea ruzuku, matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali na mchango wa Serikali kwa miradi mingine ya maendeleo.

Mhe. Spika**,** pamoja na kuendelea kusisitiza kuchukua hatua za kuimarisha mapato, Serikali pia inaendelea na hatua maalum zinazolenga kuangalia uwezekano wa kubana matumizi kwa kazi za kawaida bila ya kuathiri utendaji. Lengo ni kuwa kama kuna fedha zitakazookolewa, fedha hizo zitumike kwa kazi za maendeleo. Kwa sasa, zoezi la kufanya mapitio ya majukumu ya kila Wizara/Taasisi linaendelea. Kukamilika kwake kunatarajiwa kusaidia kuongeza ufanisi kupitia marekebisho ya kitaasisi na kuepusha mgongano wa kimajukumu.

**MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO**

Mhe. Spika, moja ya lengo la Serikali ni kuhakikisha utulivu wa mfumo wa kodi ili uwe wenye kutabirika na hivyo kuvutia wawekezaji. Hatua za kuongeza kodi huchukuliwa pale tu inapokuwa ni lazima. Kwa upande mwengine, sasa hivi, kuliko ilivyokuwa kwa wakati mwengine wowote ule, haja ya kupunguza utegemezi wa wafadhili inajitokeza. Changamoto zinazojitokeza kutokana na athari ya msukosuko wa kiuchumi na fedha katika eneo la Ulaya na kukua kwa mahitaji ya huduma kwa wananchi na dhamira ya Serikali ya kuimarisha ubora wa huduma hizo kunapelekea haja ya kuimarisha zaidi mapato yetu ya ndani. Kwa kuzingatia mambo yote haya muhimu, na ili kuziba nakisi ya bajeti katika mwaka ujao wa fedha 2013/14 kama nilivyoeleza awali, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya sheria na viwango vya kodi na ada mbalimbali kwa kurekebisha Sheria zifuatazo:

(i) Sheria ya *VAT*, namba 4 ya mwaka 1998.

(ii) Sheria ya Kodi za Hoteli namba 1 ya mwaka 1995.

(iii) Sheria ya Ada za Bandari namba 2 ya mwaka 1999.

(iv) Sheria ya Ushuru wa Stempu namba 6 ya mwaka 1996.

(v) Sheria ya Kodi za Mafuta namba 7 ya mwaka 2001.

(vi) Sheria ya Usafiri wa Barabara namba 7 ya mwaka 2003 na Kanuni zake.

(vii) Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (*Presumptive Tax Scheme).*
(viii) Sheria ya Ardhi namba 12 ya mwaka 1992.
(ix) Sheria ya Kuvutia na Kulinda Vitega Uchumi namba 11 ya mwaka 2004.
(x) Sheria ya Usimamizi wa Kodi namba 7 ya mwaka 2009.
(xi) Sheria ya Rufaa ya Kodi namba 1 ya mwaka 2006.

**A. Marekebisho ya Sheria ya *VAT***

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio ya uwekezaji katika sekta ya utalii na mchango wake mkubwa katika uchumi wa nchi yetu, bado kumekuwa na udanganyifu katika ulipaji wa kodi zinazotokana na sekta hii.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kumsikiliza Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, baadhi ya Wawekezaji wameendelea kudanganya kuhusu kiasi wanachopaswa kulipa kwa kutaja kiwango kidogo cha kutozea kodi kwa mahoteli. Pamoja na hatua mbalimbali za kisheria na kiutawala zilizochukuliwa na Serikali ili kurekebisha hali hii, bado kuna fursa ya kuimarisha zaidi mapato hayo ikiwemo kwa kudhibiti zaidi msingi wa kutozea kodi. Kwa mnasaba huo, inapendekezwa kurekebisha kiwango cha usajili wa mahoteli katika kodi ya *VAT* kwa kuzisajili tu hoteli zinazofikia kiwango cha chini cha usajili wa *VAT* na zenye kutoza ada ya huduma kuanzia USD 100 kwa mtu kwa siku (au sawa na thamani hiyo kwa Shilingi za Kitanzania). Hoteli nyengine zote zisizofikia kiwango hicho zitalipa Kodi ya Hoteli, *Hotel Levy*.

Mhe. Spika**,** nchi nyingi zinapata tabu juu ya udhibiti wa udanganyifu katika misamaha ya kodi. Serikali imekuwa ikichukua jitihada za kudhibiti misamaha ya kodi lakini bado kuna fursa ya kudhibiti zaidi. Chini ya utaratibu wa sasa wa Kodi ya Ongezeko la Thamani VAT, Serikali hutoa unafuu kwa Taasisi mbalimbali chini ya Jadweli la Tatu la Sheria ya *VAT*. Ili kukabiliana na udanganyifu na kuimarisha zaidi udhibiti wa misamaha, inapendekezwa kupunguza unafuu unaotolewa kwa baadhi ya Taasisi. Unafuu wa asilimia 100 ubakie tu kwa ofisi za Kibalozi na Miradi yenye ufadhili wa Washirika wa Maendeleo, vifaa na huduma zinazostahili. Kwa Taasisi nyengine zote zinazostahiki msamaha huo chini ya Jadueli hilo unafuu utolewe kwa asilimia 80 tu ili kiasi kilichobakia cha asilimia 20 kilipiwe kodi.

Kwa kuzingatia na hatua nyengine za kiutawala zitazochukuliwa katika *VAT*, hatua hiyo inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa TZS 4.56 bilioni.

**Marekebisho ya Sheria ya Kodi za Hoteli**

Mhe. Spika, sambamba na marekebisho ya Sheria ya *VAT*, inapendekezwa pia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi za Hoteli kwa kutoza kodi kwa kuzingatia hadhi ya hoteli. Inapendekezwa kuwa hoteli zote zinazotoa huduma kwa kiwango kisichozidi Dola za Kimarekani *US$* 40 kwa mgeni kwa siku ziendelee kulipa *VAT* kwa kiwango maalum yaani *specific*. Hata hivyo, inapendekezwa kupandisha kiwango hicho kutoka *US$* 5 kwa mtu kwa siku ya sasa hadi *US$* 8. Hoteli zilizobakia zinazotoza zaidi ya *US$* 45 lakini hazitimizi sifa ya kusajiliwa chini ya *VAT* zitaendelea kutozwa Kodi ya Hoteli kwa kiwango cha asilimia 18 kama ilivyo sasa. Marekebisho haya yanatarajiwa kuiingizia Serikali jumla ya Shs 2.86 bilioni.

**Kurekebisha Sheria ya Ada ya Viwanja vya Ndege**

Mhe. Spika, marekebisho yanayopendekzwa kufanywa katika Sheria hii yanalenga kuleta uwiano baina ya kiwango kinachotozwa Zanzibar cha ada ya uwanja wa ndege na viwango vinavyotozwa katika nchi nyengine za Afrika ya Mashariki. Inapendekezwa kupandisha ada hiyo kutoka *US$* 35 kwa mtu iliyopo sasa hadi *US$* 40 kwa mtu kama ilivyo kwa nchi jirani za Afrika ya Mashariki. Marekebisho haya yatagusa tu wasafiri waendao nje ya nchi. Kwa wasafiri wa ndani ya nchi, kiwango cha sasa kitaendelea kutumika kama kilivyo. Matarajio ni kwamba hatua hiyo itaongeza mapato kwa TZS 1.2 bilioni.

**Marekebisho ya Ushuru wa Stempu**

Mhe. Spika, Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ya viwango mwaka jana. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji, imebainika haja ya Serikali kuangalia tena unafuu wa kodi unaotolewa kwa bidhaa za vyakula muhimu. Kwa upande mwengine, kumejitokeza pia ugumu wa utekelezaji katika maeneo ya baadhi ya hati zinazopaswa kulipiwa Ushuru wa Stempu. Ili kuondoa kasoro zilizojitokeza, marekebisho yafuatayo yanapendekezwa:

(i) Kushusha rasmi kiwango cha Ushuru wa Stempu kwa bidhaa za mchele na unga wa ngano kutoka asilimia 3 cha sasa hadi asilimia 2;

(ii) Aidha, inapendekezwa kupanua ukomo wa kiwango cha malipo ya ushuru huu uliotolewa mwaka jana kwa mikopo ili utumike kwa hati nyengine zenye hadhi ya mikopo kama vile "*Debentures*". Kwa utaratibu huu, marekebisho yataweka kiwango cha juu cha Ushuru huu cha TZS 100,000.

(iii) kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Stempu kulingana na utaratibu wa "*Presumptive Tax*" kama unavyopendekezwa hapa chini.

Mhe. Spika, sambamba na marekebisho hayo ya sheria, Serikali kupitia *ZRB* inakusudia kuchukua hatua kadhaa za kiutawala zikiwemo za kuanzisha ofisi za *ZRB* katika Mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja ili kuweza kuhudumia kwa karibu zaidi walipakodi waliopo katika maeneo hayo na kutoa uwakala wa zuio la Ushuru wa Stempu *withholding Tax* kwa hoteli mbalimbali. Tayari *ZRB* inazo ofisi katika miji ya Chakechake, Wete na Mkoani kwa Pemba. Kwa pamoja hatua hizi zinategemewa kuingiza jumla ya TZS 600.0 milioni.

**Kuimarisha utaratibu wa utozaji kodi ya mafuta**

Mhe. Spika, kumeendelea kuwepo upotevu wa mapato ya Serikali kupitia magendo katika biashara ya mafuta. Hatua hii haiwezi kuachwa iendelee. Serikali kupitia *TRA*, *ZRB* na vikosi vya ulinzi itafanya operesheni maalum na ya kudumu ya kudhibiti magendo na vituo visivyo rasmi ya kuuzia mafuta. Aidha, ili kudhibiti uingiaji wa mafuta ya magendo, makubaliano ya msingi yamefikiwa baina ya *TRA/ZRB* na Mamlaka ya Mapato ya Kenya *KRA* ya kuanzisha utaratibu rasmi wa kubadilishana taarifa za uingizaji wa mafuta. Lengo ni kuzuia udanganyifu unaofanywa na waingizaji wasio waaminifu na hivyo kuchangia katika kuwepo kwa magendo. Matarajio ni kwamba hatua hizi zitaongeza mapato ya *TZS* 5.0 bilioni. Sambamba na hatua hizo, ili kuzuia uwezekano wa udanganyifu na kuhakikisha kuwepo kwa bidhaa hiyo muhimu kwa muda wote, Serikali itafanya upembuzi yakinifu juu ya uwezekano na utaratibu bora wa kuwa na muingizaji mmoja tu wa mafuta *single importer*, kama ilivyokuwa kabla.

**Marekebisho ya utaratibu wa malipo ya leseni ya njia**

Mhe. Spika, moja ya msingi muhimu wa kutoza kodi ni kuwa kodi ilipwe kwa kuzingatia matumizi na faida inayopatikana kutokana na matumizi ya huduma husika *benefit principle*. Utaratibu wa sasa wa malipo ya matumizi ya barabara hauzingatii msingi huu muhimu na unawezesha kuwepo kwa leseni bandia za njia na hivyo kuikosesha mapato serikali. Ili kukabiliana na kasoro hizo, inapendekezwa kubadilisha utaratibu wa ukusanyaji wa ada hiyo kwa kuiingiza katika mafuta. Kwa kuzingatia wastani wa matumizi ya kawaida na bila ya kumuongezea mzigo mtumiaji wa kawaida wa barabara, inapendekezwa kutozwa TZS 35 kwa lita ya dizeli au petrol itakayouzwa nchini kama leseni ya njia. Kwa kuwa kiwango hicho hakitaongeza mapato *revenue neutral*, hatua hiyo inatarajiwa kuongeza mapato kwa TZS 124

milioni tu kutokana na udhibiti wa leseni bandia na ucheleweshaji wa sasa wa malipo.

**Marekebisho ya viwango vya malipo ya leseni za udereva**

Mhe. Spika, kwa muda sasa Zanzibar imekuwa ikitumia leseni za kisasa za udereva ambazo gharama za utengenezaji wake zimeendelea kupanda. Ili kufidia gharama zinazotumika kutayarisha nyaraka za leseni za udereva na leseni hizo za kisasa kuwa endelevu, inapendekezwa kurekebisha kiwango cha leseni za udereva kutoka *TZS* 15,000 hadi *TZS* 20,000 kwa leseni ya mwaka mmoja, *TZS* 25,000 hadi *TZS* 30,000 kwa leseni ya miaka miwili na *TZS* 35,000 hadi *TZS* 40,000 kwa leseni ya miaka mitatu. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa *TZS* 120 milioni.

**Kuweka utaratibu wa kusajili magari mara tu yanakapoingia nchini**

Mhe. Spika, kutokana na kuimarika kipato cha wananchi na biashara, kumejitokeza kushamiri kwa biashara ya magari hapa nchini katika sehemu mbalimbali. Kwa bahati mbaya, kumejitokeza mtindo wa baadhi ya watu kutembelea magari hayo bila ya kutiwa nambari za usajili. Tabia hii ikiachiliwa inaweza kuathiri usalama wa watumiaji wa barabara yaani *safety* na pia kuongeza vitendo vya uhalifu. Ili kukabiliana na hali hiyo, kuanzia mwaka ujao wa fedha, vyombo vya moto vitasajiliwa mara tu vinapokamilisha taratibu za Forodha na kabla ya kutoka bandarini. Sambamba na hatua hiyo, mambo yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Kuongeza kiwango cha usajili *registration* wa vyombo vya moto kutoka TZS 50,000 hadi TZS 70,000, na hivyo kuongeza mapato kwa TZS 288 milioni; na

(b) Ili kuepusha kurundikana sana kwa nambari zisizotumika kwa magari yaliyokusudiwa kupitia tu nchini kwa ajili ya biashara, kuanzisha namba maalum kwa vyombo vya moto vinavyoingizwa kwa kusafirishwa nje ya Zanzibar kibiashara. Hatua hiyo itaongeza mapato ya Serikali kwa TZS 347.

**Sheria ya Kodi ya Mapato 2004 *Presumptive Tax Scheme* (*PTS*)**

Mhe. Spika, moja ya eneo ambalo limekuwa likilalamikiwa sana ni utaratibu wa kutoza kodi kwa wafanyabiashara wadogowadogo katika sekta isiyo rasmi. Wengi wa wafanyabiashara hawa hawana uwezo wa kuweka kumbukumbu zinazohitajika kutozea kodi ya mapato na Ushuru wa Stempu.

Serikali inahitaji kuwalea wafanyabiashara hao na kuwapunguzia mzigo wa kutimiza matakwa ya taratibu za kodi. Utaratibu unaotumika katika nchi nyengine, ikiwemo Tanzania Bara, ni kuwatoza kodi wafanyabiashara kama hawa kwa utaratibu wa *"Presumptive Tax"* ambao ni mwepesi zaidi kuufata kwani unaunganisha kodi ya mapato na ushuru wa Stempu na hauhitaji wafanyabiashara kuwasilisha Marejesho *returns* kila mwezi. Hadi sasa utaratibu wa *PTS* kwa Zanzibar unatumika kwa kuwatoza kodi ya mapato wamiliki wa magari ya biashara tu (taxi, daladala, gari za kukodisha na za mizigo).

Inapendekezwa kutumia utaratibu huo wa *PTS* kuanzia mwaka ujao wa fedha kwa wafanyabiashara ambao mauzo yao kwa mwaka hayazidi *TZS* 10 milioni. Wafanyabiashara wote watakaotozwa kodi chini ya utaratibu huu hawatalazimika tena kulipa Ushuru wa Stempu. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato kwa TZS 400 milioni.

**Marekebisho ya Misamaha ya Kodi**

Mhe. Spika, kwa muda mrefu SMZ imekuwa ikitumia vivutio mbalimbali ili kushajiisha uwekezaji binafsi nchini. Moja ya sababu ya kiwango cha vivutio vilivyopo ni kasoro mbalimbali za kisoko *market distortions* zilizokuwepo wakati huo hasa katika kukosekana miundombinu ya msingi kama vile barabara za lami, umeme na maji katika maeneo yote ya uwekezaji. Hivi sasa hali imebadilika kwani tayari miundombinu hiyo inapatikana katika takriban maeneo yote ya uwekezaji na kupelekea kupatikana mafanikio makubwa katika uwekezaji katika sekta ya utalii hususan ujenzi wa hoteli. Haja inayojitokeza sasa ni kupanua uwekezaji katika maeneo mengine muhimu ya kiuchumi ambayo hayajapata msukumo mkubwa kama vile viwanda na kilimo. Ili kuimarisha mapato ya serikali na kuweza kuvutia uwekezaji katika maeneo mapya ya viwanda na kilimo, mambo yafuatayo yanapendekezwa:

(i) Kurekebisha Sheria ya *ZIPA* kwa kufuta misamaha ya Kodi kwa vifaa vya ujenzi na vyengine vidogovidogo kwa miradi yote ya hoteli na mikahawa. Msamaha utaendelea kutolewa kwa vifaa vya uwekezaji *capital goods* kama vile mashine na vifaa vyengine vikubwa vya uwekezaji;

(ii) Kuandaa na kutoa unafuu maalum kwa uwekezaji katika viwanda, kilimo na uwekezaji wenye umuhimu maalum *Strategic Investment* kama utakavyowekewa utaratibu hapo baadae;

(iii) Ili kuzuia udanganyifu wa thamani ya uwekezaji unaopelekea kuonekana kiwango kikubwa cha misamaha, kusamehe asilimia 80 tu ya mapato kwa misamaha yote ya

watu binafsi, taasisi za kidini, *NGOs* na uwekezaji. Kiasi kilichobakia kitakusanywa.

Hatua hizi zinatarajiwa kuiingizia Serikali jumla ya TZS 5.4 bilioni.

**Kuimarisha Mapato kutokana na Ukodishaji wa Ardhi**

Mhe. Spika, Zanzibar ni kisiwa kidogo na hivyo ardhi yake ni rasilimali muhimu sana. Serikali imekuwa ikikodisha ardhi yake ili iweze kutumika kwa shughuli za uwekezaji ili kuendeleza uchumi na jamii. Watu wengi wamekuwa wakihoji udogo wa viwango vya kodi ya ardhi vinavyotumika Zanzibar. Pamoja na udogo wa viwango hivyo, Serikali pia imekuwa ikisamehe kodi kwa kipindi chote cha ujenzi wa mradi. Ili kuweza kunufaika zaidi na rasilimali hii muhimu, inapendekezwa yafuatayo kuhusiana na kodi ya ardhi:

(i) Kuyatambua na kuyaweka katika "*database*" maeneo yote ya ardhi yaliyokodishwa;

(ii) Kurekebisha viwango vya kodi kwa kuweka uwiano kwa matumizi yanayofanana kwa kuzingatia mahali lilipo eneo na matumizi yake;

(iii) Kuweka viwango maalum vya kuvutia uwekezaji katika maeneo ya vipaumbele vya viwanda, kilimo na miradi maalum *strategic investments*; na

(iv) Ili kuondoa mtindo wa maotoe katika kukodi ardhi speculation na kuhakikisha inatumika vyema kwa maendeleo ya uchumi, kufuta utaratibu wa kutoa muda wa msamaha kwa matumizi ya ardhi *grace period*. Anaekodishwa atalazimika kuanza kuilipia mara tu baada ya kukodishwa.

Mwaka ujao wa fedha unatarajiwa kuwa wa kujipanga zaidi na usimamizi ili uwezeshe kupatikana makisio sahihi ya kodi baada ya kuimarishwa usimamizi. Hata hivyo, hatua hizi zinatarajiwa kuiongezea Serikali mapato kwa angalau TZS 500 milioni.

**Hatua za Kiutawala**

Mhe. Spika, pamoja na hatua zilizopendekezwa hapo juu, bado taasisi za ukusanyaji za *TRA* na *ZRB* zitaendelea kuchukua hatua nyengine za kiutawala na utendaji zikiwemo za kuwatambua na kuawasijili walipakodi wapya,

kusimamia maeneo yaliyoonesha udhaifu kama vile mikataba ya ukodishaji wa hoteli bila ya kuwepo dhamana, matumizi ya "*tax clearance*", kusajili Washauri wa Kodi *Tax Consultants* na kugomboa kodi zilizo mikononi mwa walipakodi. Inatarajiwa kuwa hatua hizi zitaongeza mapato kwa TZS 500 milioni.

Kwa jumla hatua zote zinazopendekezwa zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa TZS 16.9 bilioni.

## SURA YA MAPATO KWA MWAKA UJAO WA FEDHA 2013/2014

### Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, kwa mwaka ujao 2013/14 Serikali inakusudia kuongeza juhudi ya ukusanyaji mapato yafikie asilimia 22.1 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 21.3 ya mwaka 2012/13. Katika mwaka ujao wa fedha, mapato kutokana na vyanzo vya ndani yanakadiriwa kufikia TZS 324.6 bilioni. Kitaasisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* inakadiriwa kukusanya TZS 147.9 bilioni, Bodi ya Mapato Zanzibar *ZRB TZS* 171.7 bilioni, TZS 5.0 bilioni gawio kutoka Benki Kuu na Mashirika ya SMZ, TZS 26.0 bilioni zitazokusanywa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kama Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar na mkopo wa ndani wa TZS 25.0 bilioni. Zikichanganywa na TZS 5.0 bilioni za kuanzia mwaka, jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia TZS 380.6 bilioni

### Misaada ya Nje

Mhe. Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2013/2014 inatarajia kupata jumla ya TZS 277.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha. Kati ya fedha hizo, TZS 235.4 bilioni ni kwa ajili ya Programu na Miradi ya Maendeleo ikiwemo TZS 148.6 bilioni za Mikopo na TZS 86.8 bilioni za ruzuku. Misaada ya kibajeti *GBS* inatarajiwa kufikia TZS 40.0 bilioni ikihusisha TZS 26.5 bilioni za ruzuku na TZS 13.5 bilioni ambazo ni mikopo. Kiasi kilichobakia cha TZS 2.5 bilioni kinatokana na salio la sehemu ya mgao Zanzibar kutokana na Msamaha wa Madeni *MDRI*.

Mhe. Spika, muundo wa Mapato unaojitokeza hapo juu unamaanisha kuwa utegemezi wa bajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, unaopimwa kama uwiano wa ruzuku kwa jumla ya matumizi, utaendelea kupungua hadi kufikia asilimia 17.2 mwaka 2013/2014 kutoka asilimia 21 mwaka 2012/2013. Aidha, uwiano wa ruzuku kwa Pato la Taifa unatarajiwa kupungua hadi kufikia asilimia 8.5 kwa mwaka wa 2013/2014 kutoka asilimia 11.2 mwaka

2012/2013. Ni muhimu kuendelea kuhakikisha kuwa mapato ya ndani yanakuwa kwa kasi zaidi kuliko ile ya ruzuku.

Mhe. Spika, mukhtasari wa mfumo wa Bajeti ya mwaka 2013/14 baada ya hatua mbalimbali za mapato na mgawanyo wa matumizi ni kama unavyoonekana katika Jadweli hapa chini.

Mfumo wa Bajeti ya mwaka 2013/14

| Maelezo | Makisio 2012/13 | Makisio 2013/14 | Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|
| MAPATO | | | |
| A. Mapato ya ndani | 294.1 | 324.6 | 10.4 |
| B. 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS) | 39.9 | 40.0 | 0.3 |
| C. Dhamana za Hazina/Hati Fungan | 15.8 | 25.0 | 58.2 |
| D. Kodi Mapato kwa w/kazi wa SMT | 0.0 | 26.0 | |
| E. Bakaa ya bajeti 2012/13 | 5.9 | 5.0 | -15.3 |
| F. Msamaha wa Madeni (MDRI) | | 2.5 | |
| G. Mikopo na Ruzuku | 293.2 | 235.4 | -19.7 |
| Jumla ya Mapato | 648.9 | 658.5 | 1.5 |
| MATUMIZI | | | |
| Matumizi ya Kawaida | 307.8 | 353.1 | 14.7 |
| i) Mishahara (Mawizara) | 139.6 | 155.5 | 11.39 |
| ii) Mishahara (ruzuku) | 17.7 | 20.8 | 17.5 |
| iii) Matumz mengineyo (Wizara) | 71.1 | 80.6 | 13.3 |
| iv) Matumizi mengineyo (ruzuku) | 26.6 | 31.2 | 16.9 |
| v) Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS) | 52.8 | 65.0 | 23.1 |
| Matumizi ya Maendeleo | 341.1 | 305.4 | -10.5 |
| i) Mchango wa Serikali | 47.9 | 70.0 | 46.1 |
| ii) Washirika wa Maendeleo | 293.2 | 235.4 | -19.7 |
| Jumla ya Matumizi | 648.9 | 658.5 | 1.5 |

*Chanzo: Idara ya Bajeti - ORFUMM*

Mhe. Spika, sura hiyo ya Bajeti ndiyo inayokusudiwa kutekeleza Mpango wa Maendeleo na kuendesha kazi za kawaida kwa mwaka ujao wa Fedha. Inatarajiwa kuwa utekelezaji wa Bajeti hiyo utupeleke karibu zaidi na kufikia malengo ya Mipango yetu Mikuu ya Maendeleo ikiwemo Dira ya 2020, MKUZA II, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Malengo ya Kimataifa yakiwemo Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Shukran.

**SHUKURANI**

Mhe. Spika**,** makadirio haya yasingeweza kuwasilishwa leo hii hapa bila ya mchango wa watu na Taasisi mbalimbali. Naomba niwashukuru wachache kwa niaba ya wengi waliochangia mafanikio ya hatua hii muhimu. Mosi, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Rais, ambae pia anaisimamia Ofisi yake hii ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Makamo wa Kwanza na wa Pili wa Rais, Wajumbe wote wa Baraza la Mapinduzi ambao ni Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote kwa kuipitia na kuitolea Muongozo Rasimu ya Bajeti hii. Shukrani pia kwa Wajumbe wa Tume ya Mipango kwa kazi kubwa ya kuzingatia na kuridhia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Spika, pili, naomba kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa uongozi wako mahiri na wa busara kwa Baraza hili. Ni kwa busara, uvumilivu na uongozi wako ndio tumeweza kuhakikisha utulivu hapa Barazani na baina ya Baraza na mihimili mingine ya Dola. Nakushukuru sana Mhe. Spika. Naomba nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza lako, Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango na muongozo wa Kamati yake. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu na Wajumbe wao kwa kukaa na Wizara zote na kupitia Mapendekezo ya Bajeti zao na kuyatolea muongozo unaofaa. Kwa hakika, Mheshimiwa Spika, nalishukuru sana Baraza lako lote kwa mchango wake katika maandalizi ya Bajeti hii.

Mhe. Spika, nje ya Baraza Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru Makatibu Wakuu na Watendaji wengine wote wa Wizara na Taasisi zinazojitegemea, Mikoa, Manispaa na Halmashauri za Wilaya. Nathamini na kuushukuru pia mchango wa Sekta binafsi na Asasi zisizo za kiserikali katika maandalizi ya Bajeti hii. Vikao vingi vimefanyika na ushauri wao umesaidia sana kufikisha Bajeti katika muundo wake wa sasa.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Rais – Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Nawashukuru sana Katibu Mkuu ndugu Khamis Mussa Omar, Katibu Mtendaji Bi. Amina Khamis Shaaban, na Naibu Katibu Mkuu ndugu Juma Ameir Hafidh.

Nawashukuru pia Kamishna wa Bajeti, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Kamishna wa Mipango ya Kitaifa, Sera za Kisekta na Kupunguza Umaskini, Kamishna wa Ukuzaji Uchumi, Kamishna wa Fedha za Nje na Wakuu wa Idara na Watendaji wote wa Ofisi yangu kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa umahiri na kujitolea hadi kufikia hatua hii. Ninapowasilisha Mapendekezo haya leo hii nafarijika kujua kuwa Mapendekezo haya ni matokeo ya kazi kubwa, ya umakini na ya juhudi ya pamoja ya Wasaidizi mahiri wanaofanya kazi kwa mashirikiano makubwa na kulitumikia Taifa letu kwa nguvu na uwezo wao wote.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru sana Washirika wetu wa Maendeleo, nchi marafiki na Mashirika ya Kimataifa, kwa mchango wao mkubwa kwa juhudi zetu za kuwaletea maisha bora wananchi wenzetu. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wazanzibari wote, naomba kuzishukuru sana nchi zote zilizosaidia na zinazoendelea kutusaidia ili nasi tupige hatua za maendeleo. Miongozi mwa nchi hizo ni Canada, China, Cuba, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea, Kuwait, Marekani, Misri, Norway, Oman, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uturuki.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mashirika ya Kimataifa, naomba kuyashukuru sana ACBF, ACRA, AfDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM BANK ya CHINA, EXIM BANK ya KOREA, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMW, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, KUWAITI FUND, MCC, NORAD, OFID, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, UN AIDS, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, USAID, WB, WHO, WSPA.

Mhe. Spika, mwisho, na kwa namna maalum, naomba kwa dhati kabisa kuwashukuru sana Wananchi wote wa Zanzibar kwa imani yao kwa serikali na Watendaji wake na Baraza lako hili. Bila ya imani ya Wananchi, leo hii kazi zetu zingeweza kufanyika, bila ya utulivu wao sote tusingeweza kuwa makini na bila ya ridhaa yao, sote tusingekuwepo. Kwa mara nyengine tena, nawaomba Wananchi wote waendelee kushirikiana nasi waliotutuma kuwatumikia ili kwa pamoja tuweze kuleta maendeleo ya nchi yetu na sisi wenyewe na kizazi chetu.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, tunaendelea kupata mafanikio katika ukuzaji wa uchumi wetu na uimarishaji wa huduma mbalimbali za jamii. Hata hivyo, lazima tubaini kuwa kazi iliyo mbele yetu ya kuleta maendeleo kwa nchi yetu na jamii yake ni

kubwa sana. Tunahitaji kujituma kwa jitihada na maarifa zaidi, sote kwa pamoja, serikalini na sekta binafsi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kwa heshima na taadhima, Baraza lako tukufu lipokee, kujadili na hatimae kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2013/14 kwa kuzingatia Mwelekeo wa Hali ya Uchumi. Kama nilivyosema, Bajeti ya mwaka ujao wa fedha ni Bajeti ya Huduma za Jamii kwa Wananchi wa Zanzibar. Serikali inapendekeza mbele ya Baraza lako tukufu kukusanya mapato ya Shilingi mia sita na hamsini na nane bilioni na mia tano milioni (TZS 658.5 bilioni). Serikali pia inapendekeza kutumia kiasi hicho cha Shilingi mia sita na hamsini na nane bilioni na mia tano milioni (TZS 658.5 bilioni) ikiwemo Shilingi mia tatu na hamsini bilioni na mia moja milioni (TZS 353.1 bilioni) kwa kazi za kawaida na Shilingi mia tatu na tano bilioni na mia nne milioni (TZS 305.4 bilioni) kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukuwe nafasi hii kwa kumshuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa kuwasilisha na hatimae kutoa hoja juu ya Hotuba ya Serikali ambayo amemaliza hivi punde kuiwasilisha mbele ya Baraza hili Tukufu.
Nawashukuru pia Waheshimiwa Waajumbe kwa kuwa na utulivu muda wote ambao Mhe. Waziri alikuwa anawasilisha Bajeti iliyochukuwa muda takriban saa moja na dakika ishirini.

Baada ya hayo na kabla ya kumkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi ili amalizie utaratibu uliobaki. Naomba kwanza niwatambue sasa rasmi wageni wetu ambao wameshirikiana na sisi katika hotuba ya leo ya bajeti. Tulialika wengi lakini waliofika kwa leo ni kama ifuatavyo:-

Naomba Waheshimiwa Wajumbe nitambue kuwepo kwa Mhe. Mama Asha Balozi Seif Idd, Wawakilishi wa Mashirika na Taasisi za Kimataifa zilizopo hapa Zanzibar.

Naomba niwatambue na wasimame kwa pamoja Makatibu Wakuu wa Wizara mbali mbali waliopo. Pia Manaibu Makatibu Wakuu ambao pia wamealikwa katika kikao hiki. Pia niwatambue Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama, kuwepo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hapa Zanzibar. Naomba pia kwatambua Wawakilishi mbali mbali kutoka kwenye Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali kama wapo naomba wasimame. Inaonekana wamepata dharura.

Waheshimiwa wageni wetu karibuni sana nakushukuruni sana kwa kuhudhuria kwenye Kikao hichi rasmi cha Bajeti ya Serikali.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba pia nitoe tangazo fupi, nimeombwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe wale wenye Majimbo kwamba wanatakiwa kupeleka jina la *Account* zao na namba za *Account* hizo kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi ili maombi yale yanayohusiana na masuala ya *PDF* yaweze kutekelezwa muda unakwenda.

Kwa hivyo, maombi hayo yanatakiwa yatekelezwe na kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe mnatakiwa mpeleke majina ya *Account* hizo pamoja na nambari za *Account* hizo kupitia kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa wajumbe kwa ujumla niwashukuru na niwashukuru watendaji wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano makubwa ya maandalizi ya Kikao hichi na mara baada ya kutoka humu ndani niwaombe Waheshimiwa Wajumbe na wageni wetu wote waliohudhuria kukusanyika hapa nje kutakuwa na dhifa ndogo ambayo imeandaliwa maalum kwa ajili ya Kikao hichi cha leo cha Bajeti.

Sasa baada ya hayo naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili atuelezee utaratibu na utamaduni wetu kwa mara baada ya kusoma Bajeti ya Serikali tupate muda wa siku mbili ambao tukajikite kidogo katika kuangalia na kuchambua Bajeti hii.

Mhe. Waziri wa Nchi njoo basi utuwekee utaratibu kwa mujibu wa kifungu cha 94 kifungu kidogo cha 5 ili kuweza kupata kutoa hoja ya kuakhirisha shughuli zetu kwa muda wa siku mbili karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa mujibu wa shughuli zetu za leo tayari Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo ameshawasilisha Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 20013/20014; na kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wanahitaji muda wa kuipitia hotuba hii ili wapate nafasi nzuri ya kuja kuichangia kwa ukamilifu wake;

Basi kwa sababu hiyo, Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu liweze kuahirisha kikao chetu hichi mpaka siku wa Jumatatu tarehe 17/06/20013, saa 3: 00 barabara asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 11.34 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 17/06/2013 saa 3:00 asubuhi)*